


# Kanisa juu ya MWAMBA

## Kujenga Kanisa kwa njia ya Kitume

### Kanisa kama linavyoendeshwa leo, litaweza kusimama kukabili mashinikizo ya mwisho wa dahari?

Kijitabu hiki ni mwongozo mkuu wa mafunzo wa **Gospel For Africa**, kiliandikwa awali hasa kwa ajili ya viongozi wa Kanisa katika Afrika ili kuelewa namna gani makanisa yatende kazi kulingana na msingi wa Kibiblia uliotolewa na Mitume.

Kanisa vile limeacha mafundisho ya Kitume, pamoja na onyo kutoka kwa Mtume Paulo katika
**2 Timotheo 4:1-4**, kwamba Kanisa litafika wakati "watakapoyakataa mafundisho yenye uzima" katika siku za mwisho, imekuwa kusudio la msingi kwa ajili ya kuandaa mwongozo huu.
Kila msomaji angekuwa mwenye busara ili kujipima kwa uangalifu msingi ambao anajenga juu yake **(1 Wakorintho 3:10-15**), ajitahidi kujionyesha kuwa amekubaliwa na Mungu **(2 Timotheo 2:14-16)** na kuutimiza wokovu wao wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka **(Wafilipi 2:12-18).**

Toleo la lugha la zamani limetumika pamoja na Kamusi za Kiebrania na Kigiriki.

**TAFADHALI** tumia Mwongozo huu ukiwa pamoja na Biblia yako ili kutazama na kuthibitisha maandiko yote yaliyorejewa.
Watu wafuatao wamechangia katika uandaaji wa kitabu hiki:

Bradley Field
Bradley Schmidt
Elijah Okeyode
Michael Mafie
Scott Wheeler

Kitabu hiki kimetolewa kwa wale wote ambao wamebaki kuwa waaminifu kwa mafundisho ya Yesu Kristo kama yalivyotolewa kwa Mitume na pasipo haya wamehubiri Injili hii wakikabiliana na upinzani mkubwa.

## UTANGULIZI

Kanisa juu ya Mwamba ni mwongozo rahisi wa kimaandiko ambao umewekwa pamoja kwa umakini kupitia maombi, ili kuleta msingi imara wa kimaandiko unaomfanya YESU KRISTO KAMA MSINGI PEKEE WA KWELI WA KANISA.

Kwa kuzingatia zaidi ufunuo wa Mtume Paulo ambao aliupokea moja kwa moja kutoka kwa Bwana Yesu Kristo mbinguni. Mwongozo huu utatoa uelewa sahihi hatua kwa hatua kwa ajili ya mtendaji wa Kikristo aliyedhamiria kujenga Kanisa JUU YA MWAMBA YESU KRISTO.

Ni mwongozo wa kipekee ambao unajumuisha mada mbalimbali muhimu zinazohitajika ili kuanzisha Kanisa la kweli. Mungu abariki Neno Lake na kuleta ongezeko katika kazi Yake kupitia kiasi anachompa kila mtendaji atakayetumia MWONGOZO huu.

- **Christopher Allan Scott,**
**Coastal Assemblies of God**

# Kanisa juu ya
# MWAMBA

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| Sura ya 1: | Nini maana ya Kanisa? | 6 |
| Sura ya 2: | Tunajengaje Kanisa? | 9 |
| Sura ya 3: | Kanisa litendeje kazi? | 11 |
| Sura ya 4: | Huduma katika Kanisa | 25 |
| Sura ya 5: | Karama za Roho | 38 |
| Sura ya 6: | Kila Mwamini ni Kuhani | 46 |
| Sura ya 7: | Vipi kuhusu Wanawake? | 48 |
| Sura ya 8: | Fungu la Kumi & Utoaji katika njia ya Mungu | 50 |
| Sura ya 9: | Nidhamu katika Kanisa | 56 |
| Sura ya 10: | Tabia iliyotengenezwa na Mungu | 61 |
| Sura ya 11: | Kitengo Imara cha Familia | 76 |
| Sura ya 12: | Nini kinatokea Mwisho? | 81 |

**Scan these QR Codes for access to more information:**

**Gospel for Africa** **Church on the Rock**

*Sura ya 1*

# NINI MAANA YA KANISA

Strong Greek Lexicon; **G1577**

ἐκκλησία

ekklēsia

*ek-klay-see'-ah*

Kutokea kwenye mjumuisho wa G1537 na ufafanuzi wa G2564; kuitwa, ni, (kushikamanishwa) mikutano mbalimbali, hasa kutaniko la kidini (Sinagogi la Kiyahudi, au washirika wa jumuiya ya Kikristo duniani au watakatifu mbinguni au wote): - kusanyiko, kanisa.

Neno ‘Kanisa (Church)’ linaonekana mara 80 katika tafsiri ya Biblia ya Kiingereza ya ‘King James Version’.
**Neno Kanisa kwa kifupi linamaanisha “walioitwa”**

**KUELEWA MAANA**
Kwa kifupi tu, ‘Kanisa’ ni kikundi cha watu ‘walioitwa’.
**Ingawa lipo katika ulimwengu kimwili, sio la ulimwengu kiroho.**

**Yohana 17:16-18**
**Kundi hili la watu, “walioitwa” ni “Kanisa” la kweli la Yesu Kristo.**
Kanisa sio jengo linaloonekana, taasisi, shirika, dhehebu, au chochote kilichotokana na mwanadamu.
“Kanisa” ni maskani ya Mungu katika roho yasiyo ya ulimwengu huu ingawa bado yanadhihirishwa ulimwenguni ili kudhihirisha utukufu wa Mungu.
**Tuangalie kile Mungu anachosema kuhusu “Kanisa” lake:**

1. Mungu hakai katika maskani au jengo linaloonekana
   **Matendo. 7:48-50 & Matendo 17:24-25**

2. Sisi ni Hekalu la Mungu
   **1 Wakorintho 3:16-17, 1 Wakorintho 6:19-20 & 2 Wakorintho 6:16**

3. Sisi ni Maskani ya kiroho
   **1 Petro 2:5**

4. Yesu ni kichwa cha "Kanisa" lake, ambalo ni mwili wake
   **Waefeso 1:22-23, Wakolosai 1:18, Warumi 12:4-5 & 1 Wakorintho 12:12, 15**

Kwahiyo, Kristo hajatenganishwa na "Kanisa" lake bali ni kitu kimoja na Yeye kama "Kichwa".
**1 Wakorintho 6:15-17**
Tukiwa pamoja na Kristo tumekuwa Roho mmoja.
Hili linatokea mara "tunapobatizwa katika Yesu Kristo" na "kuzaliwa mara ya pili".

**KUBATIZWA KATIKA KRISTO**
**Warumi 6:3, 1 Wakorintho 12:13 & Wagalatia 3:27**

**KUZALIWA MARA YA PILI**
**Yohana 3:3-7**
Ninapomwamini Yesu Kristo na kuliitia Jina lake kwa ajili ya Wokovu, ninabatizwa katika mwili wake na Roho wake anaingia ndani yangu.
Huu ni mchakato wa kiumbe kipya kujazwa na Roho wa Kristo.

**2 Wakorintho 5:17 & Luka 5:37-38**
Ni "Kiumbe Kipya" (Kiriba Kipya) pekee aweza kupokea "Roho wa Kristo" (Divai Mpya).
Hivyo kila "aliyezaliwa mara ya pili" ameumbwa tena (Kiumbe Kipya) na Mungu, na amefanywa kuwa kiungo katika "Mwili" (Kanisa) ambao anaishi ndani yake kwa "Roho Wake".

Hivyo basi, Kanisa ni maskani ya kiroho, sio tena ya ulimwengu bali ni uumbaji mpya wa Mungu uliopo ulimwenguni ili kuonesha utukufu Wake.

Kuwa kiungo katika Kanisa lake ni muujiza, ni zawadi kubwa ambayo mwanadamu aweza kuipokea na ni mwito mkuu wa kuufuata. Tumevuka kutoka kuwa wa “kitambo tu” hadi kuwa wa “Milele”; tumekuwa watenda kazi pamoja na Kristo katika kujenga “Hekalu” la Mungu la milele.

*Sura ya 2*

# TUNAJENGAJE KANISA

Hivyo basi, kanisa linajengwaje, ni nani wajenzi na linajengwa kwa kutumia nini?

**1 Wakorintho 12:4-6**

Mungu ambaye ni wa "Utatu"; Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanashiriki kikamilifu katika ujenzi wa Kanisa.

Baba (Mungu): **tofauti za kutenda kazi - Matendo 2:41-47**
Mwana (Bwana): **tofauti za huduma - Waefeso 4:7-16**
Roho Mtakatifu (Roho): **tofauti za karama - 1 Wakorintho 12:7-11**

**TOFAUTI ZA KUTENDA KAZI**

**Matendo 2:42-47**

Katika siku ya Pentekoste Petro alihubiri na watu 3,000 "wakazaliwa mara ya pili", "wakabatizwa" na mara wakaingia katika "tofauti za kutenda kazi";

1. Fundisho la Mitume
2. Ushirika
3. Kuumega Mkate
4. Kusali

**TOFAUTI ZA HUDUMA**

**Waefeso 4:11-16**

1. Mitume
2. Manabii
3. Wainjilisti
4. Wachungaji
5. Waalimu

## TOFAUTI ZA KARAMA

**1 Wakorintho 12:7-11**

1. Neno la Hekima
2. Neno la Maarifa
3. Imani
4. Karama za Kuponya
5. Matendo ya Miujiza
6. Unabii
7. Kupambanua Roho
8. Aina za Lugha
9. Tafsiri za Lugha

Ni kupitia “Kutenda Kazi, Huduma na Karama” kama ilivyoorodheshwa hapo juu, Yesu alisema katika **Mathayo 16:18**, juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

Yote haya ni ya Mungu; mwanadamu anafanyika tu chombo ambacho Mungu anakitumia kwa nguvu zake za Kiungu.

*Sura ya 3*

# KANISA LITENDEJE KAZI

1. Fundisho la Mitume
2. Ushirika
3. Kuumega Mkate
4. Kusali

Kumbuka “Kanisa” ni nyumba ya kiroho hivyo yaweza tu kujengwa kwa kutumia nyenzo za kiroho.
Kwa “kuzaliwa mara ya pili” tunavuka kutoka “kuwa wa-asili ya kawaida na kuwa wa rohoni”, na hii inakuwa ni pambano kwetu kwa kuwa tumeishi katika “asili yetu ya kawaida” na sasa tunakuwa na mpito ili kuwa wa “kiroho”.
Mungu hutuwezesha katika mapito ili kuingia katika “Utendaji Kazi Kiroho” kupitia “Fundisho la Mitume”.

**FUNDISHO LA MITUME**
Hili ni fundisho lililopokelewa moja kwa moja kutoka kwa Yesu na kufundishwa na Mitume (Mitume 12, na Paulo).

Mitume 12 waliokuwa na Yesu;
**Matendo 1:2-3**

Walipokuwa wakichagua Mtume ili kujaza nafasi ya Yuda, vigezo vifuatavyo vilitakiwa kufikiwa:
**Matendo 1:21-26**

Paulo alikuwa ni Mtume aliyechukuliwa hadi Mbinguni na kupewa ufunuo moja kwa moja na Yesu.

**2 Wakorintho 12:1-7 & Wagalatia 1:11-12**

Mitume wana jukumu la kuweka msingi "Yesu Kristo".
**1 Wakorintho 3: 10-11, Waefeso 2:20 & Waebrania 6:1-3**

"Msingi" huu unaitwa "Mafundisho ya Kwanza" ya "Fundisho la Kristo".
**Waebrania 5:12, 6:1**

Yesu ndiye "Msingi", tumefundishwa na Mitume kama "Mafundisho ya Kwanza ya Kristo".
Kwa hivyo,"Mafundisho ya Kwanza" ni "mawe katika msingi" ambayo "Fundisho" linajengwa juu yake.
Kulingana na Paulo, Petro na mwandishi wa 'Waebrania'; kila mwamini mpya (mtoto mchanga) anahitaji "Maziwa ya Neno" (Mafundisho ya Kwanza) ili kukua kabla ya kuweza kutumia "Chakula Kigumu" (Kutenda Kusudi la Mungu).

**1 Wakorintho 3:1-3, 1 Petro 2:1-2 & Waebrania 5:12-14**
"Maziwa ya Neno" ni "Mafundisho ya Kwanza / Msingi" (mawe yanayoweka msingi) ambayo yanakuwa jukwaa la "mtoto mchanga" mwamini (mwenye tabia ya mwilini / asiyejua sana neno la haki) aweze kukua na kuweza kukitumia "Chakula Kigumu" (kuwa mtu mzima / Kiroho), ambaye anaweza "Kupambanua Kusudi la Mungu".

Na hivyo, ni wazi kutokana na maandiko haya kuwa kila mwamini mpya na mwenye "tabia ya mwilini" (ambaye bado anafikiri katika asili ya kawaida au ambaye bado yupo kimwili na sio kiroho) anahitaji kuwekwa msingi katika "mafundisho ya kwanza" ambayo yatawapa

waamini wapya uwezo wa kutambua na kisha kulitenda “Kusudi la Mungu”.

Yesu anatuambia kuwa “Chakula Chake” ni kutenda “Mapenzi ya Baba Yake” na kuimaliza kazi yake.

**Yohana 4:31-34**
Hivyo basi, “Chakula Kigumu” sio kufahamu ‘mafundisho magumu ya Neno’ bali ni “Kutenda Kusudi la Mungu”.
Pasipo msingi wa “Maziwa” kamwe hatuwezi kuingia katika kuyatenda mapenzi ya Mungu “Chakula”.

Yesu anaweka namna hii katika **Mathayo**
**Mathayo 7:21-27**

Hivyo ni wazi kuwa ili kuingia katika Ufalme wa Mbinguni inatupasa tuyatende “mapenzi ya Mungu”, haitoshi kitu kusema tu, “Bwana tumefanya kazi hizi zote”.
Anaweka kauli hii ya mwanzo kabisa katika jambo hili la kujengwa juu ya “Mwamba” (Msingi / Mafunzo ya Kwanza / Maziwa).
Ni muhimu kwamba kila mwamini aimarishwe katika “Mafunzo ya Kwanza” ili aweze kutambua mwenyewe “Kusudi” la Mungu katika maisha yake.
Kufanya “matendo au kazi mbalimbali” kwa ajili ya Mungu kwa Jina lake sio kitu tunachopaswa kuweka shabaha yetu bali katika kuyatambua na kutenda mapenzi ya Mungu, “Kusudi lake”.

Katika **Waebrania** tunapewa orodha ya “Mawe ya Kujengea” yanayoufanya msingi kuwepo;
**Waebrania 6:1-2**

1. Kuzitubia kazi zisizo na uhai
2. Kuwa na imani kwa Mungu
3. Mabatizo
4. Kuwekea mikono
5. Kufufuliwa wafu
6. Hukumu ya milele
7. Kuendelea hadi utimilifu

***MAFUNDISHO YA KWANZA – KWA UJUMLA***

Utangulizi:

**2 Timotheo 2:19**
Msingi wa Mungu unatuthibitishia kuwa tu wake.
Mathayo 7: 21-27

Hekima ni kujenga katika msingi ulio sahihi, sio tu kuifahamu Biblia na kujihusisha katika shughuli za Kikristo.
Kila tunachoamini na kukitenda kitapimwa, kile tu kilichojengwa juu ya Yesu kitasalia.

**Mathayo 16: 13-18**
Baba wa Mbinguni alimfunulia Petro kwamba Yesu ni nani, ni ufunuo huu kutoka kwa Baba unaotujenga katika mwamba. Kufahamu Biblia haitoshelezi, lazima macho yetu yawe yamefunguliwa kumtambua vema Yesu.

**Waefeso 2:19-22**
Msingi huu unawekwa na Mitume na Manabii kulingana na uwezo waliopewa na Mungu.

**1 Wakorintho 12: 28**
Inaweka wazi utaratibu wa kazi kuhusu ujenzi katika Kanisa.

Mungu ameweka;
Wa **kwanza - Mitume**, wanaweka msingi.
Wa **pili - Manabii**, wanatutia moyo kujenga juu ya msingi.
Wa **tatu - Waalimu**, wanatufundisha fundisho sahihi kutokana na msingi uliowekwa.

**1 Wakorintho 3: 1-3**
Mtume Paulo anaweka wazi kuwa mkristo "mwenye tabia ya mwilini" (mtoto mchanga, mwamini mpya, ambaye bado hajakomaa, mwenye ufahamu wa kawaida tu) anahitaji "Maziwa ya Neno" (Msingi) ili kukua hadi kukomaa kiroho.

**1 Petro 2: 1-2**
Mtume Petro anafundisha hivyo hivyo.

**Waebrania 5: 12-14**
Mwandishi wa Waebrania anathibitisha jambo hili na kisha anautaja "Msingi" kama "Mafundisho ya Kwanza ya maneno ya Mungu" na kisha anaweka wazi kila fundisho la msingi.

**Waebrania 6: 1-3**
Msingi una mafundisho ya kwanza 7.
Mafundisho haya ya kwanza ni ufunuo wa Yesu Kristo kama ulivyotolewa kwetu na Baba aliye Mbinguni.

1. **Kuzitubia kazi zisizo na uhai:**

Asili ya zamani imekuwa katika hali ya kutenda "kazi / matendo" ili kuhesabiwa haki kulingana na vile inavyopewa msukumo wa hatia ya dhamira.
Mungu atatutoa katika hatia ya dhamira kupitia imani katika kazi toshelevu ya Yesu.
Mungu hakubali kazi ambayo inatokana na hatia kwani inatokana na msukumo mbaya na unatafuta kujihesabia haki na tokeo la mwisho ni utukufu wa mwanadamu.

**Waebrania 9: 11-14**
Mungu ataondoa kabisa dhamira yangu kutoka katika “Matendo Mafu” na kuniwezesha kumtumikia Mungu aliye hai.

**Waefeso 2:8-10**
Wokovu ni kwa “Neema” tu (uwezesho wa Kiungu) unaopatikana kwa njia ya “Imani” tu (kuamini tu katika utoaji wa Mungu – Yesu).

**Warumi 4: 1-5**
Ibrahimu alihesabiwa “Haki” kwa imani na sio kwa matendo au kazi.

WOKOVU UMETOLEWA BURE – NIPO HURU KUMTUMIKIA BWANA

2. **Kuwa na imani kwa Mungu:**

Kuwa na imani katika utoshelevu wa Yesu kutanifanya kujisalimisha kwa kazi ya Roho ndani yangu ambayo itazaa matunda “Kazi Njema” ambayo inakubaliwa na Mungu.
Kuwa na imani kwa Mungu kutaendelea kuniongoza ndani zaidi katika Roho na kunitoa kabisa katika matamanio yangu ya kawaida na kujitukuza mwenyewe.

**Waebrania 11: 6**
Ni “Imani” tu ndiyo inampendeza Mungu.

**Waefeso 2: 8-10**
“Imani” inazaa “Kazi Njema” kwa kuwa sasa mimi ni “Kazi yake”.

**Yakobo 2: 17-18**
“Imani ya kweli” wakati wote itadhihirishwa kwa “Kazi Njema”.
Ninapojikabidhi kwa Mungu, ananitumia kama chombo kwa ajili ya utukufu Wake.

**Wagalatia 2: 20**

"Imani" inasababisha Kristo ndani yangu kuishi kupitia mimi.
Naacha kuishi maisha yangu na Yesu anadhihirisha maisha yake ndani yangu.

**Warumi 10: 17**
"Imani" huja kwa kusikia Neno la Mungu.

**Waebrania 11: 7**
Kwa sababu Nuhu alimwamini (Imani) Mungu, alijenga safina na kwa hivyo alimpendeza Mungu.
Matokeo ya Imani ya Nuhu ilikuwa ni kazi ya Mungu na siyo uwezo wa Nuhu, na hivyo Mungu alipata utukufu.

IMANI INASABABISHA KAZI YA MUNGU NDANI YETU NA KUPITIA SISI

3. **Mafundisho ya Mabatizo:**

**Waefeso 4: 5**
Ubatizo huu "wa KWANZA" ni ubatizo katika Kristo na kutokea hapo nyingine 3 zinafuata.
Bila ubatizo huu wa kwanza, zinazofuata zinakosa maana au hazitawezekana.

- *Ubatizo katika Yesu Kristo*

Tunapomwamini Yesu "tunazaliwa mara ya pili", kiroho tunabatizwa katika Kristo.
Tunakuwa viungo katika "Mwili" Wake ulio hai, na sio viungo vya taasisi.
Kwa sababu nipo ndani ya Kristo, anaweza kuishi ndani yangu kwa Roho Wake (Divai mpya katika Kiriba kipya).

**Warumi 6: 3-4**
**Wagalatia 3:27**

**1 Wakorintho 12:13**
**2 Wakorintho 5:17**

WOKOVU – KIUMBE KIPYA

- *Ubatizo katika Maji*

Unatia muhuri wokovu wangu kwa tamko au ukiri wa nje kuhusu kilichotokea ndani.
Hili ni tamko kwamba nimefanywa mwenye "Haki".
**Mathayo 3:13-17**
**Mathayo 28:18-20**
**1 Petro 3:18-21**

UKIRI WA NJE KUONESHA BADILIKO LA NDANI – KUPATA HAKI YOTE

- *Ubatizo katika Roho Mtakatifu*

Kuyaishi maisha niliyokiri kuwa nitayaishi, nitaweza tu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.
Roho Mtakatifu anafanya karama 9 ziwepo kwa ajili ya ufanisi katika huduma.
**Luka 24:49**
**Matendo 1:8**
**Yohana 14:12-16**
**Yohana 15:26**
**Yohana 16:7-15**

NGUVU YA KUWA SHAHIDI WA YESU

- *Ubatizo katika mapito magumu ya Yesu Kristo*

Kwa sababu Kristo sasa anaishi kupitia mimi, mara zote na kwa namna yoyote tunapokataa kufuata makusudio ya "Mwili" (tamaa na nia mbaya) inapelekea kupitia mapito magumu ya namna mbalimbali.
**Mathayo 20:20-23, 26:36-44**

**2 Timotheo 3:12**
**Wafilipi 3:10**
**1 Petro 4:1-2**
**Waebrania 5:7-8**

KUACHA KUSUDI LANGU NA KUJISALIMISHA KABISA KATIKA KUSUDI LA BABA - UTII

4. **Kuwekea Mikono:**

Ikiwa kama matokeo ya mabatizo, unakuwa chombo ambacho Mungu atadhihirisha uhai wake.
Unakuwa kiungo kitendaji katika "Mwili wake ulio hai", na hii ni utendaji wa nje katika kutimiza huduma aliyoiweka ndani yako.
Sasa wewe ni kiungo katika "Mwili wa Kristo" (Kanisa) kinachotenda kwa ufanisi.

| | |
|---|---|
| **Mathayo 19:13-15** | (Kubariki watoto wadogo) |
| **Marko 16:18** | (Kuponya wagonjwa) |
| **Matendo 8:17, 19: 6** | (Kupokea Roho Mtakatifu) |
| **Matendo 6:6** | (Kutambua na kusimika huduma) |
| **1 Timotheo 4:14** | (Kupokea Karama za Roho Mtakatifu) |
| **Mathayo 10:8** | |

POKEA BURE – TOA BURE

5. **Kufufuliwa Wafu:**

Hili ni tumaini la kila mwamini, kwamba siku moja tutaachana na mwili huu unaoonekana na vikwazo vyake vyote na kisha kuvalishwa mwili wa roho usio na vikwazo.
**Yohana 5:25-28**
**Yohana 11:25-26**
**1 Wakorintho 15:12-26, 35-54**
**Wafilipi 3:11**

TUMAINI LA MWAMINI

6. **Hukumu ya Milele:**

Kuna hukumu mbalimbali za “Milele” ambazo tunahitaji kuzielewa na ambazo zinatusababisha kuishi maisha “Matakatifu”.
**Waebrania 9:27**
**1 Petro 3:18** (Yesu alihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu)
**1 Wakorintho 11:31-32** (Kujipambanua mwenyewe)
**1 Wakorintho 3:11-15** (Hukumu kwa Waamini)
**Ufunuo 20: 11-13** (Hukumu kwa wasioamini)

UWAJIBIKAJI WA MWAMINI

7. **Kuendelea hadi kuufikilia Utimilifu:**

Mungu anapokuwa amependezwa ya kuwa msingi katika maisha yako umewekwa kwa usahihi, anakuruhusu kuendelea hadi kuufikilia “Utimilifu” (Kukua / Kukomaa Kiroho).
Hili ni kusudi la Mungu kwa watoto wake wote, kwa sababu ni katika hili tunakuwa wanafunzi wa kweli na Baba anatukuzwa kwa kuwa tunazaa sana matunda – **Yohana 15:8**.
**Waebrania 10: 14**
**Wafilipi 3: 8-14**
**1 Yohana 3: 2**
**Wafilipi 2: 12**

KUHESABIWA HAKI – KUTAKASWA – KUTUKUZWA

Mara tu mafundisho haya ya kwanza yanapokuwa yamefanyika tunaanza kutambua na kuendelea katika kusudi la Mungu maishani mwetu.
Kadiri tunavyoendelea kutazama “Tofauti za Kutenda Kazi” tunaona Kanisa la kwanza liliendelea kudumu katika Fundisho la Mitume, Ushirika, Kuumega Mkate na Kusali.
Katika kazi zote zilizoorodheshwa hapa juu, utekelezaji wake waweza kuwa “rasmi au usiyo rasmi”.

Kanisa lilipoanza hawakuwa na majengo ya Kanisa, hivyo wangekutana na kutumia miundombinu iliyoko katika jamii yao vilevile nyumbani.

Siku ya Pentekoste walikuwepo watu 120 waliokusanyika pamoja katika nyumba – **Matendo 1:15**

**Matendo 2:1-2**
Walikusanyika katika Hekalu na pia nyumba kwa nyumba.

**Matendo 2:46, Matendo 5:42, Matendo 12:12, Warumi 16:5, 1 Wakorintho 16:19**
Hivyo, kutegemeana na mazingira tunamoishi na uwepo wa miundombinu ndivyo tutakavyofanya. Msisitizo usiwe kwenye mahali pa kuabudia bali katika kuona kuwa tunaendelea kudumu katika "Utendaji Kazi" uliotolewa kwetu na Mungu.
Kanisa lazima likusanyike kwa pamoja popote pale ili kufundishwa "Fundisho la Mitume".

***USHIRIKA***
Ushirika unaelezewa namna hii na Mtume Yohana;

**1 Yohana 1:1-7**
Tunapoendelea kupokea "Fundisho la Mitume" (Nuru / Ufunuo wa Yesu) na kutembea katika huo tunakuwa na "Ushirika" na Yesu Kristo na pia sisi kwa sisi.
Hivyo, "Ushirika" unatokea tunapotembea nuruni (Fundisho la Mitume), kutufikisha katika umoja pamoja na Yesu na sisi kwa sisi.
Yohana anatuambia kuwa hii itatufanya tuwe na "Furaha" timilifu.

**1 Yohana 1:4**
Kuwa katika "Ushirika" pamoja na Yesu na sisi kwa sisi inatupa kuwa katika "Furaha".
Tunafurahi sisi kwa sisi, kusanyiko letu pamoja, karama na vipawa vya kila mmoja, tunakuwa familia ambayo kuna kumpenda na kumjali kila mmoja.

Tunapokusanyika pamoja tunahudumiana, kila mmoja anamjali mwenzake, tunaombeana, tunasaidiana. Tunawahesabu wengine kuwa bora zaidi yetu.

**1 Wakorintho 12:25-27**
Kupitia "Ushirika" Kanisa linaunganishwa na kuimarishwa, kila "Anayetembea katika Nuru" atampenda mwenzake.

Hichi ndicho kinachojenga Kanisa.
**Waefeso 4:11-16**

***KUUMEGA MKATE***
"Kazi" nyingine ambayo Kanisa liliendelea kudumu kutenda ilikuwa ni "Kuumega Mkate".
Hiki sio tu kitendo cha kuwa na ushirika bali tamko lenye nguvu na muda wa kukumbuka kunakotoka katika "Ushirika" wetu pamoja.

**1 Wakorintho 10:15-23**
Kama kweli tunatembea katika nuru (Ushirika), sisi "Mkate Mmoja", tumeunganishwa kama Kanisa.
Vitu vyote ni halali, bali si vyote vifaavyo. Kila tunachofanya lazima kiwe chenye kujengana sisi kwa sisi.
Hivyo basi, huwezi kuwa mtu wa tabia fulani unapokuwa pamoja na Kanisa (wanaoshiriki Meza ya Bwana) na mtu wa tabia nyingine unapokuwa peke yako (mshiriki wa meza ya mashetani).
"Unapoumega Mkate" unatangaza kwa wote waliopo kuwa wewe ni mmoja pamoja nao, na kuwa kwa pamoja tunaufanya "Mkate Mmoja".
"Ushirika" unatufanya tuwe tumeunganishwa katika Kanisa (Mkate Mmoja).
Hivyo, tunapokuja pamoja "Kuumega Mkate" (Meza ya Bwana), tunakuja tumeunganika kama Kanisa (Mkate Mmoja) kukumbuka kazi iliyojaa utukufu ambayo Kristo aliikamilisha kwa ajili yetu.

**1 Wakorintho 11:23-33**

Paulo anaweka wazi kuwa kusudio la kuja kwetu pamoja “Kuumega Mkate” ni “Ukumbusho” wa Yesu.
Tunakumbuka gharama kubwa aliyolipa kwa ajili ya wokovu wetu, kwa kutoa uhai wake kwa ajili yetu.
Ni katika hili “Tunautambua Mwili wa Bwana” (Kanisa), tunajipima wenyewe iwapo tunafanya vivyo hivyo kila mtu kwa mwenziwe (kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya Mwili).
Tusipoweza kuupambanua Mwili wa Bwana tunakuwa na hatia ya “Mwili na Damu” ya Yesu, kwa kula na kunywa maangamizi kwetu wenyewe.
“Tusipojipambanua” wenyewe, Bwana atatrudi; “wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala”.
Anafanya hivi ili kwamba “isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia”.
Kanisa la kwanza “Waliumega Mkate” kila wiki.

**Matendo 20:7 & 1 Wakorintho 16:2**
“Kuumega Mkate” ni wakati mahususi kabisa kwa Kanisa kukumbuka alichofanya Yesu kwa ajili yetu na kujipima wenyewe katika nuru hiyo ili kuhakikisha kuwa tunafanya vivyo hivyo kwa Kanisa.
Namna hii itatuweka wakati wote katika umoja pamoja na Yesu na mtu kwa mtu, na hivyo kutufanya tusiwe wenye kujitenga wenyewe kutoka katika kundi na kupelekea kuwa shabaha ya kupatwa kirahisi na shetani. Lazima tusimame pamoja kama “Mkate Mmoja”.

***KUSALI***
Tunavyoendelea kufurahia kutembea katika nuru na kuwa na ushirika pamoja kama “Mkate Mmoja”, bila shaka tutakuwa na mzigo wa maombi kwa ajili ya kila mmoja, na kwa ajili ya wengine ili waje kushiriki jambo hili lenye utukufu ambalo linatupa furaha.

**Matendo 12:5, Matendo 4:31 & Matendo 20:36-38**
“Tofauti za Kutenda Kazi” ni mfumo wa maisha ambao Baba anataka watoto wake waingie ndani yake na waufurahie.
Mfumo huu wa maisha unatuleta katika nuru ambamo tunafurahia ushirika pamoja na Mungu na sisi kwa sisi, kutembea katika umoja na

katika huo tunashiriki furaha ambayo Baba yetu wa mbinguni anayo kwa ajili yetu.
Hili ndilo ambalo Baba amekusudia kwa Kanisa lake, ndipo sasa twaweza kuhusisha na miundo, mipango, kanuni na taratibu mbalimbali, taratibu za uvaaji, majengo, na mengine mengi.
Inapokuwa hasa ni kwa ajili ya kufurahia "Uhai" tuliopewa katika Yesu, ndio maana Paulo alisema; **Matendo 17:28-29**
Hivyo, Kanisa tangu kuanzishwa kwake liliendelea "kudumu" katika utendaji kazi wa Baba kama lilivyofundishwa na Mitume, na Mungu alikuwa pamoja nao akitenda mambo makuu na ajabu nyingi.

*Sura ya 4*

# HUDUMA KATIKA KANISA

1. Mitume
2. Manabii
3. Wainjilisti
4. Wachungaji
5. Waalimu

Kwa kadiri Kanisa linavyoendelea katika “Utendaji Kazi” uliotolewa na Baba, Yesu anatoa “Vipawa” kwa watu ili “kuhudumia” Kanisa katika “Utendaji Kazi”.
“Vipawa” hivi ni uwezo wa Bwana Yesu unaotolewa kwa madhumuni yafuatayo;
**Waefeso 4:7-13**

Paulo anafundisha kuwa hivi “Vipawa” (Huduma) ni kwa ajili ya kuwakamilisha (kukuza / kukomaza) watakatifu (waamini) kwa ajili ya kazi ya huduma (kusudi la Mungu), kujenga Kanisa.
Kutuleta katika umoja wa imani (kuamini kwa pamoja mafundisho yanayofanana) na hivyo basi kwa pamoja kufika kwenye kipimo kamilifu cha utimilifu wa Kristo (Ukamilifu wa Mungu kwa ajili yetu).
Huduma hizi sio ngazi za uongozi bali ni uwezesho wa Kiungu wa Mungu ili kuhudumia Kanisa kwa madhumuni yaliyotajwa hapa juu.

MITUME
Strong Greek Lexicon; **G652**

ἀπόστολος

apostolos

*ap-os'-tol-os*

Kutoka G649; aliyetumwa; balozi wa Injili; aliyetumwa na Kristo (mtume), (pamoja na nguvu za miujiza): - mtume, mjumbe, aliyetumwa.

“Mtume” yupo kama “Mjumbe au mtu aliyetumwa”.

Tunaona makundi 3 ya “Mitume” katika maandiko;

- Mitume waliokuwa na Yesu
- Paulo
- Mitume wengine

**Mitume waliokuwa na Yesu**
**Mathayo 10:2-3**

Baada ya Yuda kufa Mitume walimchagua mwingine wa kumi na mbili kwa kufuata msingi na vigezo vifuatavyo;
**Matendo 1:21-26**

Mitume hawa walitumwa kwa Wayahudi.
**Paulo**
Mtume ambaye hakuwa na Yesu lakini alitwaliwa mpaka mbingu ya tatu na kupokea ufunuo moja kwa moja kutoka kwa Yesu.
**2 Wakorintho 12:1-7, Wagalatia 1:11-12**

Paulo alitumwa kama Mtume kwa mataifa.
**Wagalatia 2:7-8**

**Mitume wengine**
**Matendo 14:14, Warumi 16:7 & 1 Wathesalonike 1:1-6**

Awali Yesu alichagua Mitume 12 na kuwatuma kwa Wayahudi.
Kisha Yesu akamchagua Paulo na kumtuma kwa Mataifa.
Makundi hayo 2 hapo juu walikuwa wanaume walioandika kanuni za Agano Jipya.

Mitume wengine ambao wala hawakuwa na Yesu kama wale 12 au kunyakuliwa mpaka mbingu ya tatu kama alivyokuwa Paulo, pia waliitwa Mitume, hivyo inapelekea sisi kufahamu kuwa Mitume wamekuwepo na wataendelea kuwepo katika Kanisa.

Tunaona katika maandiko huduma ya Mitume mara zote ilihusisha "Kutuma", inaweka wazi kuwa huduma hii haikuwa na kusudi la kuweka makazi ya kudumu kanisani.
Mitume walitumwa kwenye maeneo mapya ya uinjilisti, mahali Injili imepokelewa na watu waliamini walitumwa kuwaimarisha hawa waamini wapya.
**Matendo 8:5-14, Matendo 11:19-26, Matendo 13:1-4 & 1 Wathesalonike 3:12**

Paulo analiweka hili wazi kabisa "Kuweka Msingi" ni kusudio la msingi la "Huduma" yake;
**1 Wakorintho 3:10-13 & Waefeso 2:20**

Paulo pia anafundisha kuwa kuna ishara ya kuwa Mtume;
**2 Wakorintho 12:12, Matendo 2:43, Matendo 5:12 & 1 Wakorintho 9:2**

Kwahiyo tunaweza kuhitimisha kwa yafuatayo;

1. Ni huduma "iliyotumwa" kuanzisha makanisa mapya.
2. Ni huduma isiyo na makazi ya kudumu katika kanisa la mahali pamoja.
3. Ni huduma inayofanya kazi pamoja na huduma nyingine hasa "Manabii na Wazee wa Kanisa".
4. Ni huduma ya kuweka "Msingi", huubiri zaidi "Kanuni".
5. Ni huduma ambayo ina jukumu la "Uangalizi" pamoja na "Wazee wa Kanisa" juu ya makundi ya Makanisa.
6. Ni huduma inayounda sehemu ya "Wazee" (Wazee wa Kanisa) ikiwa Kanisa la mahali pamoja lina "Wazee wa Kanisa".
7. Ni huduma yenye ushuhuda wa ishara na maajabu na yenye uwezo wa kuwajenga waamini kwenye "Msingi".

MANABII
Strong Greek Lexicon; **G4396**

προφήτης

prophētēs

*prof-ay'-tace*

Kutoka kwenye mjumuisho wa G4253 na G5346; mtanguliza ujumbe (nabii); kwa mlinganisho ni msemaji aliyevuviwa; kwa uenezi ni *mshairi:* - nabii.

Kuna mkanganyiko mkubwa katika Kanisa kuhusu hii huduma.
Hitaji la kutofautisha lilifanywa kati ya haya yafuatayo;

1. Nabii wa Agano la Kale.
2. Nabii wa Agano Jipya.
3. Karama ya unabii.

**Nabii wa Agano la Kale**
**Waebrania 1:1-2**

Mfano katika Agano la Kale alikuwa Mungu "Anampaka mafuta" "Mtu binafsi" kuwa kipande cha kinywa chake; huyu alikuwa "Nabii wa Agano la Kale".
Wakati wowote watu walipohitaji kusikia kutoka kwa Mungu wangeenda kwa "Nabii".
Roho Mtakatifu aliwashukia Manabii tu na wao waliongea kwa niaba ya Mungu.
Yohana Mbatizaji alikuwa nabii wa mwisho wa aina hii;
**Luka 1:1-17**

Yesu alipokuja, Aliitwa "Kristo" (Masihi / Aliyepakwa mafuta).
**Mathayo 1:16**

Yesu alipokuja Alijazwa Roho Mtakatifu.
**Mathayo 3:16**

Yesu pia alikuwa Nabii wa watu, Mungu aliongea kupitia Yeye.

**Nabii wa Agano la Jipya**
Katika Agano la Kale Mungu aliongea kupitia manabii lakini katika nyakati za mwisho Anaongea kupitia Mwana wake.
**Waebrania 1:1-2**

Katika Agano Jipya kila mwamini anaye Yesu ndani yake kwahiyo anao "Upako" kama vile Yeye (Yesu) alivyo "Mpakwa Mafuta", na kila mwamini anaweza kujazwa Roho Mtakatifu hivyo kila mwamini anafuzu kuwa "Sehemu ya Kinywa" cha Mungu.
**1 Yohana 2:21**

Kwa hiyo hatuhitaji tena nabii wa aina ya Agano la Kale.
Nabii wa Agano Jipya ni "Mtabiri" na "Msemaji Aliyevuviwa" sawasawa na Strong Greek Lexicon.
**Matendo 11:27-28, Matendo 15:32 & Waefeso 3:2-5**

**Karama ya Unabii**
**1 Wakorintho 12:7:11**

Tutajadili hili zaidi katika sehemu inayofuata hapo chini "Tofauti za Karama".
Karama ya unabii inatolewa na Roho Mtakatifu kwa kila mtu kama Apendavyo, kwa ajili ya kulijenga Kanisa.

**1 Wakorintho 14:3**
Ni wazi kabisa "Karama ya Unabii" ni kuongea na watu ili "Kuwajenga, na Kuonya, and Kufariji".
Hii karama ni ya kuonewa shauku kwa wale wote waliojazwa na Roho Mtakatifu ili kujenga Kanisa.

"Huduma" ya "Nabii" ni kunena na Kanisa kwa "Kuvuviwa" ili kuwatia moyo waamini kuendelea kujenga juu ya msingi.

**Waefeso 2:20**

Mtu huyu anaweza pia kutumika katika “Karama ya Unabii”.

WAINJILISTI
Strong Greek Lexicon; **G2099**

εὐαγγελιστής

euaggelistēs

*yoo-ang-ghel-is-tace'*

Kutoka G2097; mhubiri wa injili: - mwinjilisti.

Tuna mfano mmoja tu katika andiko kuhusu mwinjilisti; **Matendo 21:8**
Alikuwa Filipo huyuhuyu aliyefanya uinjilisti Samaria, na akamhubiria Towashi wa Kushi katika **Matendo 8**;
Alisimikwa pia kuwa “Shemasi”.

Paulo anafundisha kuwa sisi wote tuna “Huduma ya Upatanisho” na anamtia moyo Timotheo “kufanya kazi ya Uinjilisti”
**2 Wakorintho 5:18-19 & 2 Timotheo 4:5**

“Mwinjilisti” ni mhubiri mwenye msisitizo mkuu kwenye uinjilisti.
Angehamasisha Kanisa zima kufanya kazi ya uinjilisti kwani kila mwamini anayo huduma ya upatanisho. Naye pia angefanya uinjilisti kwa ufanisi zaidi.

WACHUNGAJI
Hii huduma imekuwa na mkanganyiko mkubwa ndani ya Kanisa, imefanywa kuwa “Cheo na Nafasi” kilichotolewa kwa “Mtu Mmoja” anayechukua mamlaka ya juu kabisa katika Kanisa.
Hili sio tu tatizo kubwa lakini pia ni hatari sana na ndio sababu ya shida nyingi katika Kanisa leo.
Kuna idadi ya majina yaliyotumika kuelezea hii huduma, tutaangalia maandiko yanayohusu yote;

"MZEE"
Strong Greek Lexicon; **G4245**
πρεσβύτερος

presbuteros

*pres-boo'-ter-os*

Mlingano wa πρέσβυς presbus (*uzee*); ***mzee*; kama nomino, kiongozi**; hasa mmoja wa wajumbe wa Baraza Kuu (Sanhedrin) katika Israeli (pia ni mfano, wa mjumbe wa baraza lenye hadhi ya juu) au **Mzee wa baraza la Kikristo**: - mzee zaidi.
Strong Greek Lexicon; **G4244**

πρεσβυτέριον

presbuterion

*pres-boo-ter'-ee-on*

Sehemu tu ya ufafanuzi wa **G4245**; utaratibu wa wazee, ni, (hasa) *Sanhedrin ya Israeli* au Mzee wa Kikristo: - Mzee wa Kanisa, **mzee**.

Awepo "Mzee" kwa ajili ya kuongoza. mtu (aliyekomaa kiroho na umri), ambapo wazee wawili (2) au zaidi wanafanya "Baraza la Wazee".

Wakati wote maandiko hurejea kwa "Wazee" (Baraza la Wazee) wingi na sio umoja.
Maandiko pia yanawaweka "Wazee" katika nafasi ya "Uangalizi" (Uongozi) wa kanisa la mahali.
**Tito 1:5, Yakobo 5:14, Matendo 11:29-30 & Matendo 14:21-23**

Maandiko yanaonesha wazi kuwa "Mtume" anapokuwepo katika kanisa la mahali anakuwa sehemu katika "Baraza la Wazee" pamoja na "Wazee".
**1 Petro 5:1**

Kwa hiyo tunaona kwenye maandiko kwamba “Wazee” wanasimikwa kama “Waangalizi” wa kanisa la mahali pamoja na “Mitume” na kuunda “Uangalizi Shirikishi” juu ya makundi ya makanisa, kuimarisha umoja na fundisho sahihi, hali kadhalika kusimika wazee katika makundi ya makanisa.
Na “Mtume” anapokuwa mkazi wa kanisa la mahali anaunda sehemu ya “Wazee” pamoja na “Wazee wa Kanisa”.

“Mzee” au “Wazee wa Kanisa” pia wanaelezewa kama “Wachungaji” na “Waangalizi”.
**Matendo 20:17, 28; 1 Petro 5:1-3**

“Wazee” au Wazee wa kanisa” kwa sifa wanaweza kuteuliwa katika “Kazi ya Askofu”.
**Tito 1:5-9, 1 Timotheo 3:1-11**

Tunaweza kuthibitisha yafuatayo kutoka kwenye hayo maandiko hapo juu;
“Mzee wa Kanisa” ni ndugu kiongozi aliyepewa uwezo na Mungu kuwa “Mchungaji” wa kundi la Mungu, ambaye kwa kufikia vigezo anaweza “Kuteuliwa katika kazi ya Askofu” pamoja na Mzee mwingine mmoja au zaidi ambao kwa pamoja watachukua jukumu la “Uangalizi” wa Kanisa la mahali pamoja”.
Hili kundi la Wazee wa Kanisa “Wazee” pamoja na “Mitume” wataangalia kundi la makanisa wanayofanya nayo kazi kwa pamoja.

Sasa katika **Waefeso 4:11** Paulo anatupatia orodha ya huduma 5 zilizotolewa kwa Kanisa.
Moja ya huduma hizo ni “Mchungaji”.

MCHUNGAJI (MAELEZO YA HUDUMA HII)
Strong Greek Lexicon; **G4166**

ποιμήν

poimēn

*poy-mane'*

Ingeweza kuwekwa wazi kama; mchungaji (kihalisi au mfano): - mchungaji, kuhani.

Tumeona “Mchungaji” ni jina la huduma lililotolewa kwa ‘Shepherd’, na haya yote yana maana au tafsiri moja.

.

Kwahiyo, “Mzee wa Kanisa”, “Mzee”, “Mwangalizi”, “Askofu”, na “Mchungaji” ni wa moja na wapo sawa.

**WAZEE WA KANISA** (MAELEZO)
Strong Greek Lexicon; **G4245**
πρεσβύτερος

presbuteros

*pres-boo'-ter-os*

Ulinganisho wa πρέσβυς presbus (*uzee*), mzee**; kama nomino, kiongozi**; hasa katika Baraza la Wazee (Sanhedrin) wa Israeli (pia ni mfano wa, mjumbe wa baraza kuu) au baraza la Kikristo: - mzee, mwenye siku nyingi.

BARAZA LA WAZEE (MAELEZO YA KUNDI)
Strong Greek Lexicon; **G4244**

πρεσβυτέριον

presbuterion

*pres-boo-ter'-ee-on*

Sehemu tu ya ufafanuzi wa **G4245**; utaratibu wa wazee, ni, (hasa) *Sanhedrin ya Israeli* au Mzee wa Kikristo: - Mzee wa Kanisa, **mzee**.

**MWANGALIZI** (OFISI YA MAMLAKA)
Strong Greek Lexicon; **G1985**

ἐπίσκοπος

episkopos

*ep-is'-kop-os*

Kutoka G1909 na G4649 (katika kuhusisha na G1983); a *msimamizi*, huyu ni, afisa wa Kikristo aliye na jukumu la usimamizi mkuu wa **(au katika) kanisa** (halisi au mfano): - **askofu, mwangalizi**.

**ASKOFU** (JINA LA KAZI / OFISI)
Strong Greek Lexicon; **G1985**

ἐπίσκοπος

episkopos

*ep-is'-kop-os*

Kutoka G1909 na G4649 (katika kuhusisha na G1983); a *msimamizi*, huyu ni, afisa wa Kikristo aliye na jukumu la usimamizi mkuu wa **(au katika) kanisa** (halisi au mfano): - **askofu, mwangalizi**.

Kwahiyo, hatupaswi kutenganisha hayo majina hapo juu kwa kuleta "Vyeo, Muundo au Nafasi" kwa vile yote yanahusiana na "Huduma" moja.
Kwahiyo, "Wazee" wainuliwe ndani ya Kanisa la mahali pamoja, mahali ambapo lazima wajithibitishe wao wenyewe kwa kuonesha wana "Huduma" na kisha kuwa na sifa ya kuteuliwa katika "Kazi" mahali ambapo watachukuliana kwa pamoja na "Wazee wa Kanisa" wengine kwa jukumu la kulitunza Kanisa la mahali pamoja.
Hili kundi la Wazee wa Kanisa "Wazee" litawajibika kwa Mungu kwa ajili ya kulitunza Kanisa la mahali.

**Waebrania 13:17**

“Wazee wa Kanisa” ni “Waangalizi” wa Kanisa la mahali pamoja” hali kadhalika hufanya “Uangalizi Shirikishi” pamoja na Mitume juu ya “Makundi ya Makanisa”.
Ni “Mzee” tu ndio anayeweza kusimikwa katika “Kazi ya Askofu”
“Mitume” wanapokuwa katika Kanisa la mahali, wanasimama kwa pamoja na “Wazee wa Kanisa” husika.

WALIMU
Strong Greek Lexicon; **G1320**

διδάσκαλος

didaskalos

*did-as'-kal-os*

Kutoka G1321; muelekezaji (kwa ujumla au maalumu): - daktari, mbobezi, mwalimu.
Mwalimu ni “Muelekezaji” na aliyebobea katika hilo.

Huduma yake inasisitiza kwa wazi kwenye “Fundisho”, yeye ni “mtaalamu” (daktari) katika jambo analofundisha.
Kwa ufupi;

1. Mtume Anaweka Msingi
2. Nabii Anawatia moyo waamini kujenga kwenye Msingi.
3. Mwinjilisti Kuwaleta watu kwenye Msingi
4. Mchungaji Anawachunga waumini kwenye Msingi.
5. Mwalimu Kufundisha Fundisho la Msingi

Paulo anafundisha yafuatayo kuhusu ujenzi (usimamizi) wa Kanisa;

**1 Wakorintho 12:27-28**
Huu ni “Utaratibu” ambao huduma zinafanya kazi kwa umoja kwa kusudi la kulijenga Kanisa.

1. Mitume Kuweka Msingi.
2. Manabii Kuwatia moyo waamini kujenga kwenye Msingi.

3. Mwalimu Anawafundisha waamini Fundisho la Msingi.

Maandiko yanaweka wazi kabisa kuwa wajibu wa “Kusimamia” Kanisa hauwezi kutimizwa na “Mtu mmoja” bali ni lazima kuwepo nguvu ya pamoja kutoka katika kila huduma.
Huduma zinahitajika kufanya kazi kwa pamoja ili kumaliza kazi, kwa utaratibu uliotolewa na Mungu.
Huduma ipo ili kutenda kazi kama timu.

Kwa ajili ya ufafanuzi tu nitajadili kwa ufupi “Mashemasi”


**MASHEMASI**
Mitume na Wazee wa Kanisa wana majukumu ya wazi kabisa ya uangalizi wa “Kiroho” wa Kanisa.
Huduma nyingine 3; Manabii, Wainjilisti, na Walimu wanaweza kusimikwa katika “Kazi ya Shemasi” kama watakuwa na sifa;
**1 Timotheo 3:8-13**
“Kazi ya Shemasi” ilihitajika kwa kusudi la “Mitume na Wazee wa Kanisa” kuweza kushughulika zaidi na mahitaji ya “Kiroho” ya Kanisa, na “Mashemasi” washughulike na “mahitaji ya Kimwili”.
**Matendo 6:1-6**

Filipo aliyekuwa mmoja kati ya mashemasi 7 waliochaguliwa, alikuwa na huduma ya “Uinjilisti”.
**Matendo 21:8**

Kwa hiyo kuna “Kazi” mbili tu katika Kanisa ambazo mtu aliye na “Huduma” mojawapo aweza kusimikwa.
Kazi hizi zina sifa na vigezo vilivyo wazi na muhimu kabisa.
Hao ambao wamesimikwa katika hizi “Kazi” imewapasa wawe kielelezo katika Kanisa.

**KAZI / OFISI ZA KANISA**

# CHURCH OFFICES



*Sura ya 5*

# KARAMA ZA ROHO

1. Neno la Hekima
2. Neno la Maarifa
3. Imani
4. Karama ya Uponyaji
5. Matendo ya Miujiza
6. Unabii
7. Kupambanua roho
8. Aina za lugha
9. Tafsiri za lugha

Hizo “Karama” zilizotajwa hapo juu zinapatikana kwa kila mwamini ambaye “amebatizwa ubatizo wa Roho Mtakatifu” jambo ambalo linatokea mara baaada ya “Kubatizwa katika Yesu” (Wokovu).

**1 Wakorintho 12:7-11**

Katika 1 Wakorintho 12, Paulo anatoa matamko yafuatayo yanayohusu hizi karama;

Kwanza, Paulo anasema kuwa, “Udhihirisho wa Roho” umetolewa kwa “KILA MTU” ili “KUFAIDISHA WOTE”.

- Kwahiyo, kila mwamini anaweza “Kudhihirisha” “Karama ya Roho”.
- Pia, ni wazi kuwa “Udhihirisho” ni kwa ajili ya kufaidisha “WOTE”.

Pili, Paulo anasema kwamba Roho “Akimgawia kila mtu peke yake” “KAMA APENDAVYO YEYE”.

**1 Wakorintho 12:31**

“Kutaka sana karama zilizo kuu”, ina maana ya kuwa na **shauku ya kuwa na karama iliyo bora**.
Ni shauku ya karama **sahihi** (bora) kwa ajili ya hali au jambo fulani.
Kwa mfano;

1. Karama bora kwa ushauri wa mambo ya ndoa, ingekuwa;
    - Neno la Maarifa
    - Neno la Hekima
    - Kupambanua roho

2. Karama bora wakati wa kumuombea mgonjwa, ingekuwa;
    - Karama ya Uponyaji
    - Imani
    - Matendo ya miujiza

3. Karama iliyo bora katika kusanyiko kama wakati wa kuumega mkate, ingekuwa;
    - Aina za lugha
    - Tafsiri za lugha
    - Unabii

Kila hali inatutaka kuwa na shauku ya karama iliyo bora kwa wakati huo.
Kila mwamini aliyejazwa Roho Mtakatifu anayo fursa ya kipekee ya kutamani kuwa na karama iliyo bora ili kutia nguvu huduma.
Roho Mtakatifu anaweza kutuchagulia na kuiruhusu karama bora itende kazi kwa ajili ya lengo maalumu, na nguvu za ki-Mungu zinatuwezesha katika huduma.
Hii ndio sababu kila mwamini anahitaji kuendelea kujazwa Roho Mtakatifu na kutembea katika utakatifu mbele za Bwana ili kuweza kuwa vyombo vifaavyo kwa ajili ya kutumiwa na Bwana.
Bila kuendelea kuwezeshwa tutakosa nguvu katika huduma zetu, hii ndio sababu wengi wanageukia saikolojia na ubinadamu ili kujaribu kuhusisha mambo na saikolojia kuliko kuwa na shauku kuu ya Karama ya Roho Mtakatifu.

***Tuweke kwenye akili kuwa katika hizi karama zote ni nguvu za ki-Mungu "zenye uwezesho" wa Roho Mtakatifu. Hizi karama hazina asili ya binadamu na hazitokani na uwezo wa binadamu.***

**Neno la Hekima**

Strong Greek Lexicon; **G4678**

σοφία

sophia

*sof-ee'-ah*

Kutoka G4680; hekima (juu au chini, ulimwenguni au kiroho): -hekima.

Neno la Hekima ni "neno lililovuviwa nguvu isiyo ya kawaida inayotoka kwa Mungu" kuleta "Hekima ya Mungu" katika jambo husika.

**Neno la Maarifa**

Strong Greek Lexicon; **G1108**

γνῶσις

gnōsis

*gno'-sis*

Kutoka G1097; *kujua* (tendo), hiyo ni, (kwa kidokezo) *maarifa:* -maarifa, sayansi.

Neno la Maarifa ni "neno lililovuviwa nguvu isiyo ya kawaida inayotoka kwa Mungu" kuleta "Maarifa ya Mungu" katika jambo husika.

**Imani**

Strong Greek Lexicon; **G4102**

πίστις

pistis

*pis'-tis*

Kutoka G3982; *ushawishi*, hiyo ni, *mapokeo*; kanuni za ki-imani (ya kweli za kidini, au uaminifu wa Mungu au waalimu wa dini), hasa kumtegemea Kristo kwa wokovu; dhahania thabiti ya hii taaluma; kwa kueneza mfumo wa kidini (Injili) *ya kweli pekee yake*: - dhamana, kuamini, imani, uaminifu.

Karama ya Imani ni "uthibitisho usio wa kawaida kutoka kwa Mungu" kuleta "Imani" katika jambo au kwa mtu.

**Uponyaji**

Strong Greek Lexicon; **G2386**

ἴαμα

iama

*ee'-am-ah*

Kutoka G2390; kinga (ya athari): - uponyaji.

Karama ya Uponyaji ni "ni uwezo usio wa kawaida utokao kwa Mungu" ili kuleta "Uponyaji" katika hali fulani au kwa mtu.

**Matendo ya Miujiza**

Strong Greek Lexicon; **G1411**

δύναμις

dunamis

*doo'-nam-is*

Kutoka G1410; *nguvu* (sawasawa au mfano wa); hasa nguvu za miujiza (kawaida muujiza unaweza ukatokea wenyewe): - uwezo, utele, maana, uweza (tendo lizidio kawaida), (mtenda) muujiza, nguvu, uwezesho, vurugu, uweza (maajabu) kazi.

Kutenda Miujiza ni "ni uwezo usio wa kawaida utokao kwa Mungu" ili kuleta "miujiza ya nguvu za Mungu" katika jambo fulani au kwa mtu.

**Unabii**

Strong Greek Lexicon; **G4394**

προφητεία

prophēteia

*prof-ay-ti'-ah*

Kutoka G4396 (unabii); *utabiri* (maandiko matakatifu au mengineyo): - unabii, kutabiri.

Unabii ni "Ujumbe kutoka kwa Mungu uliojazwa nguvu isiyo ya kawaida" ili kuweza "Kujenga, Kuonya, au Kufariji" watu.
**1 Wakorintho 14:3**

**Kupambanua Roho**

Strong Greek Lexicon; **G1253**

διάκρισις

diakrisis

*dee-ak'-ree-sis*

Kutoka G1252; makadirio ya kimahakama: - kupambanua, utambuzi kwa kuweka bayana.

Strong Greek Lexicon; **G4151**

πνεῦμα

pneuma

*pnyoo'-mah*

Kutoka G4154; hewa inayotumika, hiyo ni, *pumzi* (*mlipuko*) au upepo mwanana; kwa mlinganisho au mfano wa roho, hiyo ni, (binadamu) mantiki ya nafsi, (kwa kidokezo) *kanuni muhimu*, mwenye matatizo ya kiakili, n.k, au (mwanadamu mzuri kabisa) *malaika*, *pepo*, au (uungu) Mungu, Roho ya Kristo, Roho Mtakatifu: - roho, uzima, roho, akili. Linganisha

Kupambanua Roho ni "nguvu isiyo ya kawaida itokayo kwa Mungu inayoongoza upambanuaji" ili "Kuweka wazi na kudhihirisha Roho" katika hali maalumu au kwa watu.

**Aina za Lugha**

Strong Greek Lexicon; **G1085**

γένος

genos

*ghen'-os*

Kutoka G1096; jamaa (dhahania au uthabiti, sawasawa au mfano, binafsi au mjumuisho): - kuzaliwa, nchi (-binadamu), utofauti, kizazi, uzao, taifa, vizazi, hisa.

Strong Greek Lexicon; **G1100**

γλῶσσα

glōssa

*gloce'-sah*

Uhakika wa mshikamano; lugha; kwa kidokezo lugha (hasa ambayo hakupewa kiasili):-lugha.

Aina za Lugha ni "nguvu isiyo ya kawaida itokayo kwa Mungu inayotoa lugha kutoka kwa Mungu" kwa mtu mmoja mmoja kuwawezesha kuomba moja kwa moja kutoka katika Roho na sio kwenye akili zao.
**1 Wakorintho 14:2 & Matendo 2:4-11**

**Tafsiri za Lugha**

Strong Greek Lexicon; **G2058**

ἑρμηνεία

hermēneia

*her-may-ni'-ah*

Kutoka kama ilivyo G2059; *tafsiri:* - tafsiri.

Strong Greek Lexicon; **G1100**

γλῶσσα

glōssa

*gloce'-sah*

Uhakika wa mshikamano; lugha; kwa kidokezo lugha (hasa ambayo hakupewa kiasili):-lugha.

Tafsiri za Lugha ni "ujumbe uliojaa nguvu kutoka kwa Mungu" ili "Kujenga, Kuonya au Kufariji" watu.

**Karama ya aina za Lugha ikitumika kwa mtu binafsi kwa upekee wake inamjenga mtu binafsi.**
**Lakini inapotumika Kanisani, inahitaji kufuatana na Tafsiri za Lugha ili Kanisa lifaidike kwa kujengwa.**

**1 Wakorintho 14:2-5**

**Ni wazi kutoka kwenye maandiko hapo juu kuwa "Lugha na Tafsiri" ingekuwa kama "Unabii".**

Tumetazama tayari kuhusu Utendaji kazi, Usimamizi na Karama zilizotolewa ambazo kwa hizo Kanisa linafanya kazi.
Sasa tutajadili mpango wa Mungu kwa kila mwamini kutenda kazi katika Kanisa.

*Sura ya 6*

# KILA MWAMINI NI KUHANI

Tukiongea kuhusu “Ukuhani wa Mwamini” tunarejea kwenye kanuni ya “Kila Mwamini” wa kila kanisa kuwa hai katika kutimiza “Huduma” aliyopewa na Mungu.

**Waefeso 4:1-7 & Warumi 12:3**
Kutoka kwenye maandiko hapo juu tunaona Mungu anampa kila mwamini yafuatayo;

1. “Kipimo” cha KIPAWA CHAKE KRISTO
2. NEEMA ya kubeba “Kipimo”
3. Imani ili kutimiza “Kipimo”

**Warumi 12:4-5 & 1 Wakorintho 12:12-14**
Tunaona “Mwili wa Kristo”, Kanisa, ni mwili MMOJA uliotengenezwa na viungo VINGI.
Ni kusudi la Mungu kwa kila mwamini kufanya kazi katika Mwili wa Kristo sawasawa na “Kipimo” alichowapatia.

**1 Wakorintho 12:18 & Waefeso 4:11-13**

Ni huduma tano (5) ambazo Mungu anatumia “Kumkamilisha” kila mwamini, ili kukua na kuwa mwenye ufanisi katika “Huduma”.
Kwahiyo, kila mwamini anapaswa kushiriki katika “Huduma”.
Huduma tano (5) zimepewa “Kipimo” kutoka kwa Mungu ili kuwawezesha waamini, na kuwatia nguvu ili waweze “kuzichochea” Karama ambazo zipo ndani yao.

**2 Timotheo 1:6**
Katika “Kazi” ya Kanisa kama ilivyojadiliwa katika sura ya 3, kila mwamini lazima atafute sehemu katika Mwili wa Kristo na kutumia Kipimo Mungu alichompa kwa kadiri ya uwezo kamilifu ndani yake.

Hili litatokea kulingana na **Matendo 2:42** (Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali) kama ilivyo jadiliwa katika sura ya 3.

Tunahitaji kuona kila mwamini anaendelea katika kipimo chake, ili Mwili wote kwa pamoja uweze kufika kwenye "kimo cha Utimilifu wa Kristo".
**Waefeso 4:13**

Hapa ndipo tunaweza kufurahia utimilifu wa Mungu kati yetu kama Kanisa.
Ili hili litokee, kila mwamini anahitaji kufanya kazi kwa kadiri ya kipimo chake.
Hiki ndicho walichokifurahia Kanisa la kwenye Kitabu cha Matendo ya Mitume, tunaweza kufurahia na sisi leo kama ambavyo siku zote imekuwa makusudi ya Mungu kwa Kanisa Lake.

Kwa hiyo tunaona kuwa;

1. Kila mwamini ana "Kipimo" na hivyo jambo mahususi la kufanya.
2. Huduma tano (5) ni vipimo mahususi alivyovitoa Mungu ili kuwawezesha waamini kutenda kazi ya huduma.

*Sura ya 7*

# VIPI KUHUSU WANAWAKE

Tunahitaji kuelezea mada ya “Wanawake kwenye Uongozi” ndani ya Kanisa kwani kuna mkanganyiko kuhusu hili.

**Waefeso 4:7**

Hili linajumuisha wanaume na wanawake, kwa hiyo iko wazi kutoka kwenye maandiko kwamba kila mwamini amepokea “Kipimo cha kipawa chake Kristo”.

**1 Timotheo 2:12**
Hapa Paulo anaweka wazi kuwa mwanamke HARUHUSIWI “Kufundisha au Kutwaa” mamlaka juu ya mwanaume, hivyo inawatoa wanawake kwenye uongozi.
Kama wanawake watachukua jukumu la uongozi katika Kanisa wangekuwa moja kwa moja “wametwaa” mamlaka juu ya wanaume.

Paulo pia anafundisha yafuatayo;

**Sifa kwa ajili ya kazi ya Askofu au Shemasi**
Katika sura ya 4 tumejifunza “Tofauti za Huduma” 5, hizi zote ni “Vipimo” vya uongozi kama vile “Zinavyosimamia” Kanisa.
Ni hizi huduma 5 pekee ndio zinaweza kuwa na sifa kwa ajili ya “Kazi ya Askofu au Shemasi”. Na moja kati ya sifa ni mtu lazima awe **mume wa mke mmoja**, haijafundisha kamwe kuwa anaweza kuwa ni mwanamke ambaye ni **mke wa mume mmoja**.
**1 Timotheo 3:2 & Tito 1:6-7**

**Utaratibu wa Mungu:** Mungu – Kristo – Mwanaume – Mwanamke

**1 Wakorintho 11:3, Waefeso 5:22-24 & Wakolosai 3:18**

Hii haimaanishi wanawake WASIONGEE ndani ya Kanisa bali inamaanishi mwanamke asijadili na mwanaume katika namna ambayo ni sawa na kutwaa mamlaka juu ya mwanaume.

**1 Wakorintho 14:3-35 & 1 Timotheo 2:11-12**
Tumeona tena kwenye maandiko kuwa wanawake hawawezi kuwa kwenye uongozi, na wasiingie kwenye majadiliano au hoja katika Kanisa, bali waliache jambo hili kwa wanaume, mawazo au michango yao kuhusu mijadala hiyo ifikishwe kupitia waume zao.
Wajadiliane pamoja na waume zao nyumbani na waume ambao wana “Kipawa cha Huduma” (Moja kati ya Huduma 5) wanaweza kulileta kwa Kanisa.

**Wanawake waliokuwa wasaidizi katika huduma**
Dorkasi – Matendo 9:36
Lidia – Matendo 16:13 & Matendo 16:14-15

**Sifa za Wajane**

**1 Timotheo 5:9-10, Warumi 16:1-15 & Wafilipi 4:3**
Ni wazi kabisa kuwa wanawake wengi walikuwa na mzigo kwa ajili ya INJILI na walikuwa na umuhimu sana kwenye huduma.
Wanawake wanapaswa kushiriki kwenye huduma kwa kadiri inavyowezekana ili mradi tu hawachukui jukumu la uongozi.

*Sura ya 8*

# FUNGU LA KUMI NA UTOAJI KATIKA NJIA YA MUNGU

FUNGU LA KUMI

Strong Greek Lexicon; **H4643**

מַעֲשֵׂר מַעֲשַׂר מַעַשְׂרָה

maʽăśêr maʽăśar maʽaśrâh

*mah-as-ayr', mah-as-ar', mah-as-raw'*

Kutoka H6240; sehemu ya kumi; hasa zaka*:* - ki-kumi (sehemu), utoaji zaka.

Fungu la Kumi ina maana “Kikumi”

**Utoaji Fungu la Kumi kabla ya Torati**
Utoaji “Fungu la Kumi” ulikuwa ni “Kanuni” iliyowekwa hata kabla ya Musa kupewa Torati.
**Mwanzo 14:18-20**

Hapa tunaona ni namna gani Abramu alitoa Fungu la Kumi kwa Melkizedeki, Kuhani wa Mungu, wa mfano wa Kristo.
**Waebrania 7:1-4**

**Fungu la Kumi kama lilivyoamriwa kwa Torati**
Aina 3 za Fungu la Kumi ziliamriwa na Mungu;

1. Fungu la Kumi kwa ajili ya Walawi (Sadaka ya Kuinuliwa)
   **Hesabu 18:21-24**

2. Fungu la Kumi la Mavuno
   **Kumbukumbu la Torati 14:22-27**

3. Fungu la Kumi kwa ajili ya Maskini
   **Kumbukumbu la Torati 14:28-29**

Ndipo tunaona Fungu la Kumi lilikuwa kwa ajili ya madhumuni matatu (3):

1. Walawi - Kusaidia Ukuhani
2. Watoaji Fungu la Kumi - Kufurahia kusudio lolote aliloamua Mungu
3. Maskini - Kwa ajili ya wale wasionacho

**Fungu la Kumi, alivyofundisha Yesu**

Yesu hakutoa fundisho kuhusu utoaji Fungu la Kumi bali kuhusu tabia yetu juu ya namna tunavyotoa.

**Mathayo 6:1-4, Mathayo 10:8 & Matendo 20:35**

**Utoaji Fungu la Kumi katika Agano Jipya**

Katika Agano Jipya hatuoni fundisho juu ya utoaji Fungu la Kumi, bali tunaona 'Kanuni' ya UTOAJI.

Naamini kwamba Mungu asingetaka kutuwekea mpaka kutoa "FUNGU LA KUMI" tu lakini badala yake tufanye zaidi katika utoaji wetu. Hata hivyo, Fungu la Kumi ni sehemu nzuri ya kuanzia.

Kristo ni utimilifu wa sheria, na Anaishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu.

Kama "Viumbe Vipya" tumechukua asili Yake - Upendo; zaidi ya hapo hakuna sheria.

Kwahiyo, ikiwa mimi ni kama Yesu na nafanya kila kitu kutokea katika upendo, kutoa kwangu kutakuwa sawasawa na jinsi anavyotoa; kwa Ukarimu, Utele, Kujitoa, Kwa moyo wote bila kutarajia kurejeshewa.

Kwahiyo, kutoka kwenye msingi huu tuangalie maandiko yanayohusu "Kutoa" kwetu.

**1 Wakorintho 16:1-2, 2 Wakorintho 9:6-7 & Matendo 4:32-37**

Tunaona kutoka kwenye maandiko hapo juu kuwa Utoaji lilikuwa ni tendo la kawaida katika Kanisa la Agano Jipya;

- Kama Mungu alivyomfanikisha mtu.
- Kwa kadiri ya makusudio ya mtu katika moyo wake mwenyewe.
- Sio kwa Huzuni.
- Sio nje ya kusudi
- Kwa Ukarimu
- Kwa Furaha
- Kwa Mitume

Ingekuwa sahihi kumhimiza kila mwamini kutoa kama Kristo na kutoa kama ilivyo orodheshwa hapo juu.
Tutoe kwa wingi kwa kadiri tunavyoweza badala ya kutoa kidogo iwezekanavyo.
Tusiwekewe kikomo au mpaka kwa Fungu la Kumi.
Tutoe kama kwa Bwana badala ya kulazimishwa na ili kuonekana na watu.

Tufanye nini kwa kile kilichotolewa?

- Kwanza, tunasaidia "Huduma", wale wanaotenda kazi.

  Kama tu vile Fungu la Kumi mwanzoni chini ya Torati lilivyokuwa kwa ajili ya "Walawi" (Ukuhani), hivyo basi tunasaidia kwanza wale watenda kazi katika huduma.

**1 Wakorintho 9:7-14**

Yeyote katika "Huduma tano (5)" ambaye anatenda kazi, anastahili kusaidiwa (Hili linafanyika kulingana na uhitaji, kwa makubaliano na kadiri ya upatikanaji wa fedha).
Huduma sio ajira ni "Wito" na fedha zitolewazo sio mshahara bali ni uungaji mkono tu.
Kwahiyo, kiasi kitatofautiana kati ya mtu na mtu, kutegemeana na mahitaji yao.

**1 Timotheo 5:17-18**
Tunaona uhitaji wa kuwasaidia Wazee (hasa wale wafanyao kazi ya Kuhutubu na Kufundisha) kwa vile mara nyingi watachukua jukumu la “Muda Mwingi” kuwajibika katika Kanisa.

Hivyo, baadhi yao watahitaji msaada kamili kwa sababu wamewekwa wakfu na wanajihusisha tu na kazi ya Huduma na hawana chanzo chochote cha kuwaingizia mapato.
Wengine watahitaji msaada kwa kiasi fulani tu kwani wana vyanzo vingine vya mapato.

Kuna gharama nyingine zihusianazo na “Huduma” kama;

- Eneo la kusanyiko – kukodishwa au kununuliwa
- Malazi
- Kuhusiana na Usafiri

Tumechagua namna ifuatayo;
**Matendo 2:44 & Matendo 4:32-35**

Kwahiyo basi, tunajitahidi kushirikiana kila kitu tulichonacho, hivyo, makanisa yote yanayofanya kazi kwa pamoja chini ya usajili wetu ulio rasmi kisheria ndani ya nchi watashirikisha walivyonavyo.
Kila Kanisa la mahali pamoja lina Akaunti yake ya Benki, na litatatua gharama zao za uendeshaji.
Kile kiasi kinachobaki baada ya matumizi yote katika tawi, kitumwe kwenye “Akaunti Kuu”.
Kutoka kwenye mfuko mkuu tunasaidia yafuatayo;

- Watenda kazi wote, wa muda-wote – ili pawepo na msaada wa nauli kwa wote.
- Wajane na Yatima ambao tuna wajibu wa kuwatunza.
- Ununuzi wa mali na vitu vingine vya thamani ambavyo vimewekwa chini ya “Udhamini”.
- Umisheni.

Hii akaunti imefanyika chini ya udhamini na inasimamiwa na wadhamini kutoka katika makanisa yetu mbalimbali.
“Wadhamini” ni;

- Mitume – wao wanajua mahitaji ya kazi yote.
- Wazee na Mashemasi waliosimikwa – watu ambao wametambuliwa kuwa ni wenye kufaa kati yetu kwa jambo hili.

Mitume wanashauri kuhusu mahitaji katika kazi, na Wazee pamoja na Mashemasi wasimamie mgawanyo wa fungu sawasawa na upatikanaji, hitaji la kisheria na ushauri mzuri wa kifedha.

Kuwasaidia Wajane
**1 Timotheo 5:3-16**

Tumeona kutoka kwenye andiko hapo juu kuwa sio kila mwanamke aliyefiwa na mumewe ana sifa za kuwa “Mjane Kwelikweli”.
Kwa mwanamke kuwa na sifa kama “Mjane Kwelikweli” anahitaji kufikia viwango vifuatavyo;

- Aliyeachwa mwenyewe - Ametelekezwa.
- Anamwamini Mungu.
- Awe anadumu katika maombi
- Asiyependa starehe au anasa
- Asiyelaumiwa.
- Mwenye miaka 60 na zaidi.
- Anayeshuhudiwa kwa matendo mema
- Ikiwa amelea watoto
- Mke wa mume 1
- Ikiwa amekaribisha wageni
- Ikiwa amewaosha watakatifu miguu
- Ikiwa amewasaidia wateswao
- Ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema

Ni jukumu la wana familia kuwasaidia wajane, lakini iwapo hawana ndugu au ndugu hawawajibiki kuwatunza, Kanisa litachukua jukumu hilo.

Kuwasaidia Yatima
**Yakobo 1:27**

Maandiko yanatutaka kuwatembelea Yatima katika mateso yao.
Hatuwajibiki kifedha kama Kanisa kuwatunza yatima zaidi ya kuwaonesha huruma na rehema.
Ingekuwa sahihi ki-fundisho kuwasaidia yatima kwa "Sadaka na Matoleo" kuliko Fungu la Kumi.

**Tunafanyia nini sadaka na matoleo:**
**Mathayo 10:8, Matendo 2:44-46, Warumi 12:13 & Wafilipi 2:4**

Sawasawa na maandiko yaliyotajwa hapo juu, tunahitaji kutumia "Sadaka na Matoleo" kwa mahitaji ya ndani ya Kanisa.
Mahitaji haya yanaweza kutofautiana, na kila hitaji lifanyiwe tathimini na kukubaliwa na "Wazee".
Kipaumbele chetu cha kwanza ni "Kanisa la Mahali" kisha "Kundi la Makanisa" tulio chini yake, kabla hatujashughulikia mahitaji mengineyo.
Isingekuwa vema kusaidia tu huduma nyingine yoyote, miradi n.k. kabla kwanza hatujamaliza mahitaji yetu yote, kwa sababu watu wanatoa kwa kusudi hili.

*Sura ya 9*

# NIDHAMU KATIKA KANISA

Nidhamu Kanisani haijasikika karibu kwenye makanisa mengi ya kisasa, kwasababu kwa kiasi tunakubaliana na kutekeleza kwa ajili ya usahihi wa kisiasa.
Kanisa limekuwa kama klabu za kidunia, kujaribu kuwavutia mno washirika kupitia namna mbalimbali za burudani.
Hili limeliacha kanisa katika sehemu kubwa ya kukubaliana na kutowezekana kwa kiasi kikubwa kuleta namna yoyote ya nidhamu ndani ya kanisa bila kuwaudhi watu - watu wanaolipia burudani.

Yesu anatoa tamko la kushangaza;

**Yohana 18:37**

Anatangaza kuwa kusudi lake la msingi la kuja duniani lilikuwa kushuhudia “KWELI”.
Kwahiyo, Yesu alipokuja KWELI iliingia ulimwenguni.
Kweli hiihii inahitajika kuendelezwa ulimwenguni kwa sababu ni KWELI tu ndio inaweza kuwaweka watu huru.
Paulo analiweka hili wazi katika barua yake kwa Timotheo kuwa Kanisa ni “Nguzo na Msingi wa Kweli”.

**1 Timotheo 3:15**
Ni kusudio la lazima na la msingi kwa Kanisa la Yesu Kristo kuwa KWELI katika ulimwengu huu.
Mara tu tunapopoteza kuliona hili, tunafifia.
Kwahiyo, ili Kanisa kuwa “Nguzo na Msingi wa Kweli” lazima tuhakikishe kunakuwepo nidhamu katika Kanisa.
Hivyo, Nidhamu Kanisani sio tu suala la nidhamu badala yake ni kutekeleza kusudi letu la msingi katika ulimwengu.

Kwa hiyo tunapoanzwa kutingwa na kuwa na mwelekeo tofauti ni muhimu turudishwe katika kusudi letu la msingi, hili linahitaji nidhamu.

Tupo "Mara kwa Mara" chini ya miundo mbalimbali ya nidhamu;

- "Neno" la Mungu.
- Kwa kuwa washirika wa Kanisa la Mungu.
- Kuumega Mkate.
- Kutembea katika nuru.
- Kumkemea mtu mmoja mmoja
- Kukemea kundi zima
- Nidhamu ya wengi.

Mara nyingi watu wanachanganya "Nidhamu" na "Adhabu", haya maneno hayafanani kabisa.
Mungu atawahukumu wasioamini kwenye Moto wa Jehanamu baada ya hukumu kuu kutoka Kiti cha Enzi Cheupe cha Mungu.
Mungu hutuadabisha kwa kusudi la kuturekebisha katika maisha yetu ili tuweze kufurahia utimilifu Alionao kwa ajili yetu.

**Waebrania 12:5-10 & Ufunuo 3:19**
Ni dhahiri kabisa kutoka kwenye maandiko hapo juu kuwa Mungu anatuadabisha kwa sababu Anatupenda kama watoto Wake na hatimaye kwa manufaa yetu.

**Mifano ya Jumla ya Nidhamu ya Kanisa:**

Kukiwa na mtu ametenda kosa au dhambi ndani ya kanisa, tunafuata namna ifuatayo;
**Mathayo 18:15-19**

1. Nenda kwa ndugu yako kwa kusudi la "Kumpata".
2. Kama hatakupokea na kukusikiliza, chukua pamoja nawe shahidi.
3. Kama hatawasikiliza liambie Kanisa lote.

4. Kama asipolisikiliza Kanisa, na aondolewe katika ushirika.
   Hii ndio maana ya “Mtakayoyafunga duniani”.
   Tunakubaliana kama Kanisa kuwa ndugu ameondolewa katika ushirika; tunamuomba Bwana kumtenga na ushirika na kumuadabisha kwa tumaini kuwa atatubu.
   Hili pia “Limefungwa Mbinguni”, hivyo haijalishi ndugu huyu atakwenda wapi, hayuko tena katika ushirika na Bwana. Na kisha Mungu atamuadabisha na ikiwa atatubu, twaweza kumpokea tena katika ushirika.
   Mara tunapoona matunda ya toba, tutamuomba Bwana “kumfungua” kutoka kwenye adhabu na kurejeshwa kwa upya kwenye ushirika kamili.

Ikiwa mtu ametenda dhambi ambayo ina athiri kiasi kikubwa, na kulileta aibu Kanisa na ipo wazi kwenye umma wa watu, tutafuata namna ifuatayo;

Kwa kutumia tena namna ya **Mathayo 18:15-19**, tunaiacha hatua ile ya kwanza kwani suala hili halihusu mtu mmoja kumpata mwingine.
1. “Wazee” watakutana na mtu au watu waliotenda dhambi.
2. Kutegemeana na ukubwa wa dhambi na kama imebeba nyingine wataamua ukali wa adhabu.
3. Kama “Wazee” watasikilizwa na muhusika au wahusika, hatua za kinidhamu zitafikiwa kulingana na uwepo wa “Wazee”; na iwapo “Wazee” hawakusikilizwa, suala hili lifikishwe kwa Kanisa.
4. Kama muhusika au wahusika hawatalisikiliza Kanisa, muhusika au wahusika waondolewe katika ushirika.
   Hili litafanyika kama ilivyo katika hatua ya 4 ya namna iliyopita.

Zingatia pia ukweli wa andiko lifuatalo:
**1 Timotheo 5:20**

Kwa wale watakaowapokea na kuwasikiliza “Wazee”, hatua za kinidhamu zitatolewa vile inavyostahili.
Yafuatayo yatafanyika katika namna mbalimbali za ukali na urefu wa muda;

- Vikwazo katika kushirikiana kwenye kusanyiko au vikao.
- Vikwazo katika kukutana na washirika.
- Vikwazo katika kushiriki kwenye kusanyiko - maombi, utoaji shuhuda, kuhubiri, kuongoza n.k.

Mara matunda ya toba yanapokuwa dhahiri hatua za kinidhamu zitapunguzwa taratibu na kuondolewa vikwazo vilivyowekwa mpaka vyote vitakapokuwa vimeondolewa na muhusika au wahusika wamerejeshwa kwa upya kwenye ushirika.
Ikiwa dhambi ya uzinzi au uasherati imetendwa, tunafuata namna ifuatayo;

Kwa kutumia tena namna ya **Mathayo 18:15-19**, tunaziacha hatua zile mbili za kwanza kwa sababu ya ukali wa dhambi.
Kisha tunazingatia maandiko yafuatayo;
**1 Wakorintho 5:1-13**

1. “Wazee” watakutana na muhusika au wahusika na kuwakemea na kutenga muhusika au wahusika nje ya Kanisa.
2. Kisha Kanisa litakuja kwa pamoja “KUFUNGIA” duniani, na katika suala hili sio tu kumuomba Mungu kumuondoa muhusika au wahusika katika ushirika bali pia kuondoa kabisa ulinzi wa Mungu katika maisha ya muhusika au wahusika na kuwaachilia kwa shetani kwa ajili ya uharibu wa miili yao.
3. Ikiwa muhusika au wahusika watatubu watarejeshwa katika Kanisa chini ya hatua za kinidhamu kama zilivyowekwa katika namna zilizokwisha kutajwa hapo juu.

Hivyo, tunaona katika hatua zote za kinidhamu, zinatendeka kwa makusudi yafuatayo:

1. Kulilinda Kanisa zaidi kuliko “muhusika au wahusika”.
2. Kurekebisha “muhusika au wahusika” ili waokolewa.

Chini ni maandiko machache yanayohusu dhambi inayopewa hatua za kinidhamu mbele ya watu wote;
**1 Wakorintho 6:9-10, Waefeso 5:3-6 & 1 Wakorintho 5:9-11**

Ni wazi kuna mengi zaidi mtu aweza kuzungumza kuhusu Nidhamu Kanisani vivyo hivyo kama ilivyo mada nyeti sana.
Hii ndio sababu tunahitaji busara kubwa na uongozi wa Mungu wakati wowote tunapoweka hatua za kinidhamu.
Kanisa linahitaji kufundishwa vizuri kuhusu jambo hili ili wakati hatua za kinidhamu zinatekelezwa, Kanisa linakuwa linaelewa vizuri kabisa na hakuna mgawanyiko ndani ya Kanisa.
Ni jambo nyeti sana kuwaadhibu watu wa familia moja ndani ya Kanisa.
Tunahitajika kuweka nidhamu kwa busara kubwa, neema na upendo.
Wakati wote kumbuka kuwa tunahitaji kumrudisha mtu kwenye ushirika pamoja na Kristo, kamwe "hatuadhibu" watu.
Tunahakikisha nidhamu inakuwepo kwa sababu tuna upendo;

1. Kwanza Kanisa, hatutaki lichafuke.
2. Pili muhusika au wahusika, kwani tunazitunza nafsi zao.

*Sura ya 10*

# TABIA ILIYOTENGENEZWA NA MUNGU

Tabia inaelezewa kama;

- Sifa ya asili ambayo inaelezea ukweli na uhalisia wa asili ya kitu mtu alichonacho.

  Kwahiyo, tunaelezewa kwa tabia zetu.

Kuwa na "Tabia ya Kiungu" ingemaanisha uhitaji wetu wa kufahamika kwa tabia ya Mungu.
Mf. Tunahitajika kuishi kwa tabia ya Yesu.

**2 Petro 1:2-4**
Petro analiweka hili wazi kwa kiasi kikubwa kwamba tumepewa "yote tunayohitaji" kuwa washiriki wa "tabia ya Kiungu" ya Mungu.

Tabia ni tunda la kiroho lililojengwa kutokea kwenye uhalisia wetu, uhusiano na Mungu, na kujitoa kikamilifu kwa Kristo kama BWANA. Dhamiri zetu ni nyuzi zilizotanda katikati ya ubinadamu wetu, kutuweka tayari na kuushikilia uhusiano wetu ukitiwa muhuri kama chaguo na dhamira, na sio hisia tu au haiba. Tabia inaungana na Tunda la Roho, na tabia nyinginezo nyingi za Bwana wetu ili kukuza uwezo wetu kuhusiana na kukua katika uhusiano wetu, kuwafanya wengine kuwa bora hali kadhalika na kwetu wenyewe.

**Yohana 3:30**

**Hapa kuna orodha ya tabia za Kiungu ambazo Anatuita tumuige na kuweka katika uhusiano wetu.** Hizi ni muhimu kwa ukuaji wa mahusiano yenye afya na yanayodumu. Unaweza kuchunguza maelezo, tazama kwa kina maandiko, na kisha ujiulize wewe mwenyewe haya maswali sita:

1. Hii tabia inafanya kazi ndani yangu?

2. Nawezaje sasa kuionesha tabia hii katika maisha yangu ya kila siku?

3. Nawezaje kutumia hii tabia kuendeleza utayari bora wa kuwa na mwitikio kwa wengine - hasa wale ninaowapenda - kwa hisia za kuhitaji kufanya zaidi, huku nikiwa na hofu ya Mungu, na heshima kwa watu?

4. Vikwazo gani vinavyozuia tabia hii isitende kazi na kujidhihirisha ndani yangu?

5. Nawezaje kuifanya tabia hii itende kazi vizuri zaidi, kwa uimara, na kwa haraka, hata wakati wa kutingwa na kutokuwa na uhakika, na msongo wa mawazo?

6. Fikiria kupitia hatua ambazo ungezichukua kuifanya tabia hii ifanye kazi katika mfano mahususi, au, kuiboresha. Zingatia mifano ya vifungu kutoka kwenye Neno la Mungu.

**Matunda ya Wagalatia: (Wagalatia 5:22-23)**

·**Upendo** utatusaidia kuwaona wa maana ndugu zetu wa kiume na wa kike katika Bwana, na, hata familia zetu, na wengine waliotuzunguka. Upendo ni kuchukua hatua kuinuka na kufikia mahitaji ya wengine bila kutarajia kurejeshewa kitu. **(Yohana 13:1; 15:13; 1 Wakorintho 13:3)**

· **Furaha** inaturuhusu kufurahia uumbaji Wake, wengine, na hali yetu kwa kuonesha furaha kweli, furaha halisi hutokea kutokana na mshikamano na Mungu na wengine. **(Mithali 15:13; Yohana 15:11; 17:13)**

· **Amani** kujiachilia na kujikabidhi kwa Bwana akutawale, kwani Yeye ni amani yetu kuu! Inaruhusu utulivu kuwa tendo la kutawala hasira zetu. Hili litatiwa nguvu na uhusiano wetu wa usawa na Mungu kwa hiyo tunaweza kutawala moyo wetu, kusudio, na akili zetu Kwake. Mara tutakapofanya amani ya kweli pamoja na Mungu, tutakuwa na uwezo wa kufanya na kudumisha amani kwa wengine. **(Mathayo 5:9; Wakolosai 3:15; Wafilipi 4:7)**

· **Uvumilivu** ni kuonesha kuvumiliana na kuwatia moyo wengine, na hata kukubali hali zao ngumu na bila kutengeneza madai au kuwafanya watende kama unavyotaka. **(Mathayo 27:14; Warumi 12:12; Yakobo 1:3, 12)**

· **Utu wema** kutenda kwa ukarimu na mtazamo wa ki-upendo kwa wengine. **(Waefeso 4:32)**

· **Fadhili** kuonesha uadilifu, uaminifu, na kuwahurumia wengine, na inatufanya kutenda jambo sahihi. **(Matthew 19:16)**

· **Uaminifu** ni tunda ambalo litatunza imani yetu na tabia nyingine za Roho na hata kutambua Mapenzi ya Mungu kwa hiyo tunaweza kumtegemea na kumwamini Mungu na wengine. **(Mathayo 17:19; 25:21; 1 Wakorintho 12:9; Waebrania 11:1; 1 Wathesalonike 5:24)**

· **Upole** ni tabia ambayo itaonesha utulivu, kujali, na huruma katika kushughulika na mahitaji ya wengine. **(Isaya 40:11; Wafilipi 4: 5; 2 Timotheo 2:24; 1 Wathesalonike 2:7)**

· **Kiasi** kitatupa kuwa na nidhamu, na kujizuia kwa utii kwa Mungu na wengine. **(1 Wathesalonike 5: 22)**

**Matunda mengine ya Ki-biblia:**

**Naongeza orodha hii kwani tabia ya Ki-ungu ni muhimu sana kwa uongozi.**

· **Kusamehe** ni utambuzi wa kiasi gani tumesamehewa na Kristo. Hii inatuwezesha kusamehe vitu visivyofaa tulivyofanyiwa. Hii inahusisha kutokukata tamaa juu ya wengine na kupuuza makosa tuliyotendewa, kwahiyo, tunaweza kuuponya uhusiano kwa kuelezea upendo wa Kristo. **(Luka 23:34; Waefeso 4:32; Wakolosai 3:13)**

· **Unyenyekevu** hupunguza majivuno na kuondoa kiburi. Ni kufahamu anguko letu la asili na tabia ya kujifikiria sisi ni bora kuliko jinsi tulivyo, na kutafuta kujiinua juu ya wengine na Mungu. Ni kuwakubali wengine, na muhimu zaidi ni kuona kuwa Mungu anawajibika na mafanikio yetu. Unyenyekevu utatuwezesha kuwa watu wasikivu ambao wana utayari wa kuwa chini ya wengine na kutumika, mwenye kutubu dhambi na kukumbuka jinsi Kristo alivyotumika kwa ajili yetu! **(Luka 22:27; Wafilipi 2:8; 1 Petro 5:3-5)**

· **Haki** huona hali kwa mtazamo wa kumhusisha kila mtu na sio sisi tu. Inatafuta ubora, haki, hali ya usawa, hata kama inatuumiza. **(Mathayo 7:12)**

· **Moyo wa ushujaa** hutambua kuwa Mungu ametupatia nguvu ya kuikabili hali yoyote, jaribu, au hatari. Ni uwezo wa kutoa mwitikio, kujua kuwa Mungu anatawala, na kwamba Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yule aliye kinyume na mimi. **(Kumbukumbu 31:6 & 1 Yohana 4:4)**

· **Urafiki** ni ushirika na ukaribu tulionao kati yetu. Ni kujitoa kikamilifu kusaidia kuunda tabia katika wengine. Hii siyo ya kuhofiwa bali ya kung'ang'aniwa, hata ikiwa inaumiza! **(Mithali 27:17)**

· **Uaminifu & Ukweli** ina maana ya kuwa muwazi na mkweli kwa wengine na kufanya jambo sahihi. Hii tabia itatufanya tuaminike kwa kuwa sahihi katika ukweli kuhusu mambo na hali mbalimbali. **(2 Wakorintho 8:21 & Waefeso 4:25)**

· **Kutegemewa** ni kuwa wa kuaminika na mwaminifu daima. Inatuwezesha kuendelea kujitoa kikamilifu hata kama inamaanisha kujitoa kama sadaka. **(1 Wakorintho 4:2 & Wakolosai 1:10)**

· **Shukrani** ni tabia ya kushukuru, hata tunapokuwa hatuoni tulivyo navyo. Hichi ni kipengele cha kuabudu, kueleza kwa Mungu na wengine jinsi walivyonufaisha maisha yetu kwa kuonesha msaada wao na ukarimu. **(1 Wakorintho 4:7 & 1 Wathesalonike 5: 18)**

· **Wajibu** ni kujua na kufanya anachotarajia Mungu na wengine. **(Warumi 14:12)**

· **Kuridhika** ni tabia ya kukubali na kukifurahia kile Mungu anachotupa. Haitafuti tusichohitaji kwa ajili ya kujifurahisha, na haitafuti furaha kwa vitu visivyo vya msingi katika maisha. **(Warumi 9:19-21; Wafilipi 4:10-13 & 1 Timotheo 6:6-9)**

· **Ukarimu** unatuwezesha kuwapatia wengine kwa sababu Mungu ametupatia kwa utele. Ni hekima ya kutumia uwakili na mtazamo kuwa vyote nilivyo navyo ni mali ya Mungu na kujua sisi ni watunzaji tu kwa makusudi Yake. **(Kumbukumbu 16:17 & Mathayo 10:8)**

· **Usafi & Utakatifu** ni kujitenga mbali na anasa za dunia ili Mungu akutumie, ambao ndio utakatifu kwenye matendo. Hauturuhusu kuchafuliwa au kuingiliwa na wengine katika ukuaji na uhusiano wetu na Kristo. **(Mathayo 5:8; Wafilipi 4:8; 1 Timotheo 1:5; 5:22 & Yakobo 4:8)**

· **Ujasiri** hutusaidia kumtegemea Bwana kwa kila kitu katika maisha yetu. Utatusaidia kusonga mbele kwenye mwelekeo ambao tumeitiwa kwa sababu Anatawala. Unatufanya tutambue kuwa hatuwajibiki tu kwa ajili ya matokeo – bali, utii tu. **(Wafilipi 4:13)**

· **Kutia moyo** kutatuinua, kutusaidia, na kusaidia wengine wakati wanapitia matatizo mbalimbali, mitazamo yote itoke kwa

Mungu. **(Zaburi 119:28; 143:3; Mathayo 3:17; Yohana 14:1 & 1 Wathesalonike 5:11-14)**

· **Upatikanaji** ni kuwa na utayari wa kurekebisha ratiba zetu wenyewe, ajenda, na mipango ili ifae shauku na kusudi la Mungu na wengine. Inaweka vipaumbele vya mtu binafsi kuwa vya pili na wakati wote tupatikane katika kusudi la Mungu na wengine. Ni kutazama zaidi vipaumbele vya Mungu, hivyo wakati wote tunapatikana Kwake na kwa wengine tunapotumika. **(Marko 1:17-18 & Matendo 16:10)**

· **Usikivu** utatambua thamani ya watu wengine kwa kuwasikiliza, kuwaheshimu, hisani, na kuwapa kipaumbele kwa ujumla. Hii inamaana kuwatazama wengine, na sio tu kusikiliza kwa mahitaji na shauku yetu, na pia kutafakari kwa uhakika Neno la Mungu. **(Waebrania 2:1)**

· **Hekima** ni shauku ya kweli ya kulifahamu Neno la Mungu na kulitumia kwa usahihi katika maisha yetu. Hii inatuwezesha kutoa hukumu na maamuzi mazuri. **(1 Wafalme 3:9; Zaburi 119:97-98)**

· **Huruma** itatufanya kuhisi maumivu na magumu ya wengine. Itatuwezesha kufikisha hisia zetu za upendo wa ndani kabisa ambao utatupa msukumo kukutana na hali zao ngumu, mapambano na mahitaji yao. **(Ayubu 29:13; Isaya 40:11; Marko 1:41 & 1 Petro 3:8)**

· **Shauku** inatuwezesha kushinda kuvunjika moyo na kurudi nyuma, kwa hiyo tunaweza kuwa chanya, wenye matumaini, na kuinua maslahi yetu, mitazamo, na bidii, hata kama vitu ni vigumu. **(Mathayo 5:16; Warumi 12:11; Wagalatia 6:9 & Wakolosai 3:23)**

· **Mpango** utatupa kujitambua na kujiweka katika mstari wa mbele kuona na kufanya yale yanayohitajika kabla ya kuambiwa kuyafanye. **(Mithali 22:29 & Wafilipi 3:14; 4:13-15)**

· **Bidii** inatuwezesha kutenda kwa juhudi kwa ajili ya ukuu Wake na hisia na shauku ya kumaliza kazi na wito wetu kutoka kwa Bwana. **(Mithali 10:4; Warumi 12:11 & Wakolosai 3:23)**

· **Kutafakari** kuzingatia, kusikiliza kwa umakini, kwa kujali wengine na kuziweka mbele hisia zao. **(Wafilipi 2:4)**

· **Ufanisi** ni kuwa na mpangilio mzuri, mwenye kuhimili ushindani, na kuwa mbunifu hata kuweza kutumia vema kila fursa inayojitokeza, kufanya kwa kadiri tuwezavyo na kutafuta namna bora zaidi. **(Zaburi 90:12; Waefeso 4:23; 5:15- 16; 1 Petro 4:10)**

· **Busara** hutuliza akili zetu na kutupa kufanya maamuzi sahihi, kutoa umakini wa hali ya juu katika kufikiri juu ya kinachoendelea. Itachagua kwa uangalifu maneno, hali, na matendo kuwa sahihi kwa kila hali, hivyo kuepuka maneno na vitendo ambavyo vitatusababishia matokeo mabaya. **(Zaburi 112:5; Mithali 22:3 & Warumi 12: 2, 9; 14:19, 22)**

· **Matumaini** kufikiria ubora na kuona u-chanya wa watu na hali zote, hata kama baadaye itathibitika haikuwa sahihi. **(Luka 21:18; Yohana 16:33; Warumi 8:25; 28)**

· **Utii** ni kujiachilia kufanya kile Mungu anataka tukifanye, Pia ni kutambua mamlaka na mwelekeo wa wengine, kama vile Wachungaji na Kanisa, kwa hiyo tunaweza kuleta uwezekano wa kushinda. **(Kumbukumbu 13: 4; Mithali 19:16; Yohana 14:14; 15:14; 2 Wakorintho 10:5)**

· **Heshima** ni kutambua na kuwaheshimu watu, sio tu kwa sababu ya nafasi na mamlaka yao, lakini kama ndugu katika Bwana, haijalishi haiba yao, kujua Anawapenda wote pia! **(1 Petro 2:13-14)**

· **Kukubaliana** tafuta utatuzi wa ki-Biblia na msaada kwa wengine, bila kuacha kweli. **(Amosi 3:3)**

· **Kutambua jema** kumpa Mungu shukrani za dhati kama namna ya kuabudu na kumpenda. Hii inatuwezesha kutoa, na kuwathamini wengine kwa kuwaheshimu. **(Warumi 12:10)**

· **Kuepuka hasira** kujua nguvu yake ya uharibifu na kutafuta "kuipooza" na utulivu. **(Yakobo 1:19)**

· **Kuwa mfano mwema** hii haikuruhusu uhusiano wako na Kristo kuwa wa kinafiki, watu wakiona mfano wako uwe kama vile Mkristo alivyo! **(1 Petro 2:21-25 & 1 Petro 2:12, 15, 17)**

· **Imani kama mtoto** ni ajabu na kuona thamani ya kile Kristo alichotufanyia. Ni kitu ambacho hatupaswi kamwe kukipoteza. Tudumishe juhudi zetu na tusiwe wa sehemu ya utamaduni au utaratibu fulani tu! **(Mathayo 18:2-4, 34)**

· **Kujitoa kikamilifu** ni kujiweka wakfu na kusonga mbele pamoja na kuridhika na kile ulichonacho. Ni kuahidi kuheshimu na kufanya kwa ubora wa juu kwa kutumia kile alichotupa Mungu cha kiroho na vitu vya kimwili. **(1 Timotheo 6:20)**

· **Kuwasiliana** ni kuwa na utayari wa kufikisha mawazo, mitazamo, hisia, na matendo kwa wengine kwa namna njema na kusikiliza kwa namna inayomdhihirisha Kristo. **(1 Timotheo 4:12)**

· **Imani thabiti** ni ibada kwa na kufuata maagizo ya maandiko kwa bidii, kwa gharama zozote. **(Danieli 1:8)**

· **Utayari wa kushirikiana** ni kusaidia na utayari wa kufanya kazi kwa pamoja katika amani, umoja, na mshikamano. **(Waefeso 4:3)**

· **Ubunifu** ni uwezo wa kuibua mbinu na namna bora katika kutumia vitu na vipawa tulivyopewa na Mungu ili tumtumikie Bwana. **(1 Timotheo 4:14)**

· **Juhudi** ni kupenda wito wetu na kutafuta kutimiza kazi yetu, kwa kufanya kadiri tuwezavyo kwa ajili ya utukufu Wake. **(Wakolosai 3:23)**

· **Kudhamiria** ni uwezo wa kufanya maamuzi magumu na kutimiza malengo ya Mungu kwa kuzingatia kweli ya Neno la Mungu, bila kujali upinzani. **(Zaburi 119:30 & 2 Timotheo 4:7, 8)**

· **Kustahi** ni utayari wa kuweka chini uhuru binafsi kwa ajili ya kuheshimu na kuwaona wengine kuwa bora zaidi. **(Warumi 14:21)**

· **Ibada** ni kuandaa shauku binafsi, mipango, kuabudu, na kumtumaini Mungu. **(Wakolosai 3:2)**

· **Utambuzi** ni uwezo wa kuona watu na hali kulingana na jinsi zilivyo kwa nia ya kweli na haki, huku ukichukua tahadhari pamoja na kufanya vitendo vipasavyo na katika muda sahihi. **(1 Samweli 16:7 & Mithali 19:2)**

· **Nidhamu** ni kushikilia na kuendelea kuwa mwaminifu na mpangilio mzuri wa maisha kupitia utiifu wa kiungu, bila kujali tunavyojisikia. **(1 Timotheo 4:7)**

· **Maamuzi** ni kubakia katika haki na maamuzi ya haki yenye msingi katika mapenzi makamilifu ya Mungu. **(Warumi 12:2)**

· **Usiape au kukejeli** ni kukataa kuumiza wengine kwa maneno! **(Yakobo 1:26)**

· **Ustahimilivu** ni ile nguvu ya ndani ili kubaki katika Yeye na uwezo wa kuendelea katika kulitimiza kusudi la Mungu. **(Wagalatia 6:9)**

· **Kutokuogopa** ni kuikabili hatari bila kuwa mpumbavu. **Moyo wa kiasi** ni kuwa na ujasiri kwani Mungu anatutia nguvu. **(2 Timotheo 1:7)**

· **Kupokea badiliko** ni kuwa wazi kwa mipango na mawazo ya wengine na utayari wa kuelekezwa na kupewa changamoto ili kubadilika na kuwa bora. **(Wakolosai 3:2)**

· **Vipaumbele vya ki-Mungu** ni kuchagua kufuata maagizo ya maandiko kama ratiba muhimu ya msingi na thamani ya maisha. **(Mathayo 6:33)**

· **Utauwa** ni ucha Mungu, hubadilisha vipaumbele vyetu na kuvipanga viendane na tabia ya Mungu. **(3 Yohana 1:11)**

· **Neema** ni kurahisisha na kushuka ambapo hupunguza ugumu. **(Zaburi 94:11; Yakobo 4:6)**

· **Mwongozo** ni utayari wa kuwasaidia wengine kufanyia kazi maagizo ya Maandiko kila siku na katika hali ngumu. **(Mithali 27:9)**

· **Kutokuathiri vibaya** ni kutokuwa tayari kuwaumiza wengine au kitu chochote. **(Waebrania 7:26)**

· **Kuwa mkweli** ni kusema na kutenda kile cha kweli na haki mbele za Mungu na wengine. **(Waebrania 7:26)**

· **Ukaribishaji** ni utayari wa kushirikisha, na kutambua, kile Mungu alichotupa, ikiwemo familia yetu, nyumba, fedha, na chakula. **(Warumi 12:13)**

· **Uadilifu** ni utii wa kanuni na viwango vya maadili ambazo zina heshima, kweli, na vyenye kutegemea. Inamuwezesha mtu kulishika neno lake na kufanya vema kabisa hata kama hakuna anayetazama. **(Zaburi 78:72)**

· **Haki** ni kufanya kile kilicho sawa, dhamira, bila upendeleo, na sahihi, sawasawa na mapenzi ya Mungu. **(Mwanzo 6:9)**

· **Kujitoa kwa uaminifu** ni kubaki na nia ile ile kwa wale ambao Mungu amewaletea katika maisha yetu na ametuita kutumika, hata katika kipindi kigumu. **(Mithali 17:17)**

· **Upole** haihusiani na kuwa dhaifu! Ni uwezo uliotawaliwa, ambao unatoa haki za mtu na matarajio kwa Mungu. **(Zaburi 62:5)**

· **Kurehemu** ni kuonesha msamaha zaidi, neema na wema kuliko ambavyo ulimwengu unataka. **(Luka 6:36)**

· **Subira** ni uimara wa kukubali hali ngumu za wengine ambazo hatuzipendi. Pamoja na Mungu, ni kuamini muda Wake, na tusimuwekee tarehe ya ukomo. **(Warumi 12:12)**

· **Uvumilivu** ni kutokuzimia moyo katika wito wetu, bali kuwa na uwezo wa kudumu katika kuendelea kushughulikia msongo ili kuweza kukamilisha kile Mungu alichotuitia. **(Wagalatia 6:9)**

· **Ushawishi** kuwasilisha Neno la Mungu kwa wengine ili waweze kubadilishwa mtazamo wao na kugeukia katika mapenzi Yake. **(2 Timotheo 2:25)**

· **Upesi** si kuwashikilia wengine nyuma kwa sababu ya mapungufu yetu; bali ni kuheshimu muda wa wengine na kuwa na uwezo wa kutenda kwa haraka tunapoitwa Mungu na wengine. **(Mhubiri 3:1)**

· **Kutenda kwa busara** kuweka na kutumia wema, mantiki, na haki katika maamuzi juu ya hali mbalimbali kwa namna ambayo itasaidia kuepuka makosa na matatizo. **(Mithali 13:6; 22:3)**

· **Kusudi** hii ni kujua sisi ni nani katika Kristo na kutendea kazi kwa wito wetu. Hii ni, kujitoa maisha yetu, Karama za Kiroho, uwezo, na wito ili kuleta kilicho bora katika watu na hali mbalimbali. Maana ya maisha yetu itakuwa na hazina na matokeo ya milele. **(Yohana 15)**

· **Heshima** ni kuwa mwenye nidhamu na adabu kwa watu, na mamlaka ya kiraia Mungu aliyoweka katika maisha yetu. **(1 Wathesalonike 5:13-13)**

· **Usalama** ni kumwamini na kumtegemea Mungu kwa ajili ya mahitaji yetu ya kila siku. Huu sio uvivu, bali ni kutenda kwa maadili ya ki-Mungu, na kupangilia maisha yetu katika Kusudi la Mungu na kupata hisia za mtazamo wa milele katika ufahamu. Tupo salama kwa sababu ya ulinzi wa Mungu. **(Mithali 29:25 & Yohana 6:27)**

· **Kujishusha** ni pamoja na hofu na heshima, kujisalimisha na kujitoa makusudio na mipango yetu kwa mwongozo wa Mungu. **(Waefeso 5:21)**

· **Kujikubali** ni kutambua tunapendwa sana na kukubaliwa na Kristo, hivyo, tunaweza kujikubali. Ili kuwapenda wengine, tunapaswa kujipenda wenyewe kwanza kama Kristo alivyotuonesha. Kujichukia mwenyewe sio Ki-Biblia! Kujikubali kutatuwezesha kukubali muonekano usiobadilika wa baadhi ya maumbo na hali ambazo Mungu amezitengeneza, na hivyo, tunaweza kuweka shabaha katika masuala muhimu zaidi katika maisha kama vile tabia. **(2 Wakoritho 12:9-10)**

· **Kutokuwa na ubinafsi** ni kuwajali na kujitoa wenyewe kwa wengine, kama Kristo alivyojitoa Mwenyewe kwa ajili yetu. **(Tito 2:14)**

· **Unyeti** ni kufanya wema na huruma kwa hiyo tunaweza kwenda mbali zaidi ya fikra na mantiki ya kawaida ili kuweza kuwapokea na kutoa mwitikio kwa wengine. **(Warumi 12:15)**

· **Uongozi wa Kitumishi** ni kuongoza kwa tabia ya Ki-ungu kama Kristo alivyofanya, kwa kuchukua kwake kitambaa, ushawishi, kuwaandaa, na kuwapa watu nguvu ili kutimiza kusudi na mpango wa Mungu. **(Luka 22:26)**

· **Uwazi** ni bidii ya kweli iliyo tayari kufanya kilicho cha haki, kwa dhamiri safi na yenye upendo. **(Yoshua 24:14 & 1 Petro1:22)**

· **Mafanikio** sio kile ulimwengu unasema ni mafanikio; ni kujua na kufuata kwa uaminifu Kusudi la Mungu na Neno Lake. Ni utii wetu, sio idadi yetu au vipimo vyetu! **(Mathayo 25:21)**

· **Mateso** hatuyatafuti, lakini ikitokea, hutuwezesha kugeuka na kutengenezwa ili kuwa bora kama "Kristo alivyoteseka" na kutufanya kuwa bora zaidi. Sio mashambulizi ya mtu binafsi, isipokuwa ina maana ya kutupa umakini na kutufanya kuwa bora, wenye kufaa zaidi kutumika, imara, na kufahamu kitu kinachoendelea katika maisha ya wengine**. (1 Petro 4:1-19)**

· **Kuunga mkono** kujumuika pamoja na wengine, kushirikisha uimara wetu na kuwatia moyo wanapokuwa katika mateso na taabu. **(Wagalatia 6:2)**

· **Kuwa mwenye adabu** ni kujali, kuwa mwangalifu, na kujadiliana na wengine kwa kuweka uwiano mzuri kihisia na mawazo, kufanya na kusema mambo sahihi. **(Wakolosai 4:6)**

· **Kufundisha** ni kushirikisha wengine mawazo yetu na kile tulichojifunza, kuwafanya kuwa wanafunzi. **(Mathayo 7:28; 28:19-20; Yohana 7:16; Marko 4:2; & 2 Yohana 1:9)**

· **Kuweza kujizuia** ni kuweza kujitawala ili tusipoteze mwelekeo na kuanza kuwaka tamaa na kujihusisha na maovu katika jamii. **(Tito 2:12)**

· **Kuvumilia** ni kuwa mvumilivu na kuchukuliana na wengine, hata kama wapo tofauti au dhaifu. **(1 Wathesalonike 5:14)**

· **Kufanya kwa ukamilifu** ni bidii yenye umakini ambayo inabeba wito wetu na juhudi zetu kwa ajili ya kukubaliwa na Mungu. **(Mhubiri 9:10 & Wakolosai 3:23)**

· **Muda** ni kipindi ambacho ama tunateketea au kuishi kwa utukufu Wake. Ni zile fursa tunazopaswa kuishi, kutumika, kujifunza, na kukua. Katika kufanya hivyo, kama tukiwekeza kwa hekima, tutazalisha hazina za milele. Kama sio, itapotea. **(Zaburi 90:12)**

· **Uelewa** ni uwezo wa kuhoji na kufahamu hali mbalimbali. **(Zaburi 119:34)**

· **Fadhila** ni kushikilia kanuni za maadili mazuri ambazo zinatutia katika nafasi ya juu ambayo watu wachache wana shauku ya kuifikia, lakini kama Mkristo, lazima tuende! **(Wakolosai 3:12-17)**

· **Kuwa na bidii** kudumisha juhudi yetu kwa ajili ya imani na wito wetu, na kutoliacha kanisa letu au sisi wenyewe kuangukia katika kazi iliyopoteza kusudi na yenye maneno matupu. **(Luke 2:49; Yohana 2:17, 8:29)**

Na, kuna tabia za Ki-ungu nyingi sana, zilizowekwa wazi katika Biblia, ambazo Mungu anatutaka tuzikumbatie, na kuzitenda katika maisha yetu! Kumbuka, hizi zote zinaunganishwa ili kumtengeneza, Mkristo aliyekomaa na aliyefanana na Kristo. Kile Kristo anatupa katika neema, na namna mwitikio wetu ulivyo kwa wengine waliotuzunguka ni muhimu sana katika mahusiano yetu yote.

Ikiwa viungo vingine vya uhusiano mwema vipo sawa, kisha upendo utakuja. Upendo hauwezi kusimama wenyewe, unahitaji viungo pamoja na tabia nzuri, mtazamo, na heshima, kwa hiyo tunaweza kutembea kwenye njia ya uhusiano kwa ujasiri, na kwa uhakika kuwa Kristo anaangaza njia yetu.

**UWAKILI**

**1 Wakorintho 4:1-2**
**Maisha Yote ni uwakili**; kuanzia kujifunza ukiwa mtoto, kuangalia midoli na wanyama wafugwao, kuwajali watoto wenzako katika familia, hadi kufikia kumiliki na kutunza gari na nyumba yako ya kwanza, kujitoa maisha yako kwa ajili ya mke/mume wako, na kulea watoto aliokupa Mungu.
Tunahitaji kujifunza kuwa mawakili kutokea katika ujana wetu kwani kila kitu tulichonacho tumepokea kama zawadi kutoka kwa Mungu, yote ni Yake.
Ametukabidhi vingi tuvitunze, tuwe "Mawakili Wema" ambao tutatoa hesabu mbele Zake siku moja.

Fikiria mfano huu aliosema Yesu kuhusu uwakili;
**Mathayo 25:14-30**

Kanuni ya msingi ili kuwa na tabia ya Kiungu ni uwakili, ambapo maisha yangu yote naishi kwa ajili ya "Utukufu wa Mungu". – **Yohana 15:8**

*Sura ya 11*

# KITENGO IMARA CHA FAMILIA

Sura hii imeongezwa kwa maelezo kuwa kama mtu ameitwa na Mungu, anashiriki kikamilifu katika huduma na yupo katika ndoa, anapaswa kuiweka ndoa yake katika utaratibu.
Ikiwa ndoa ya mtu imeanguka, moja kwa moja anakosa sifa za Kazi au Ofisi za Kanisa, yaani Kazi ya Askofu na Shemasi, na ushuhuda wake umeharibika. Anaweza kurejeshwa lakini hili litachukua muda na mara zote hubakiza doa katika huduma yake. Iwapo upo katika ndoa au unahitaji kuingia katika ndoa, huu ni wajibu wako wa KWANZA na MKUBWA katika huduma kabla hata hujamhubiria mtu yeyote.

Ndoa ni taasisi iliyoundwa na Mungu kwa kusudio la Mwanaume kuwa na "Msaidizi".
**Mwanzo 2:20-24**

Siyo vema mwanaume kuwa peke yake, kwa kiwango kikubwa mwanaume anahitaji "Msaidizi" – **1 Wakorintho 11:8-9**

Lakini Paulo anashauri pia kuwa mtu anayeweza "kujizuia" – **1 Wakorintho 7:7-9**, anaweza kubaki peke yake na ataweza kujitoa kikamilifu kwa Bwana – **1 Wakorintho 7:28, 32-38**.

Hivyo basi, ni wazi katika maandiko kuwa kusudio la msingi la ndoa ni kuzuia zinaa – **1 Wakorintho 7:1-6.**

Na vilevile, kufuatana na hili, ni ili kufurahia kikamilifu kusudi la Mungu la uwepo wa ndoa – **Waefeso 5:22-33**

Ndoa katika Kristo ni ujuzi wenye UTIMILIFU MKUU ambao mtu aweza kuufurahia kwa kadiri kila mmoja anavyojitoa kwa mwenzake, kuhudumiana, na kusaidiana mahitaji; Kimwili, Kihisia, na Kiroho.

Huu ni udhihirisho wenye NGUVU kwa ulimwengu kuhusu YESU na KANISA Lake.
Ndoa zetu lazima ziwe kielelezo sawasawa na picha hii.

MUNGU ANACHUKIA KUACHANA

Ikiwa ndoa ni kielelezo kuhusu Yesu na Kanisa Lake, talaka au kuachana yaweza kuwa ni alama ya kutengana kwa Yesu na Kanisa Lake. Mungu ameahidi "kutokutuacha wala kutupungukia" - **Waebrania 13:5**

Wanaume wanapaswa kuwapenda wake zao kama vile Yesu anavyolipenda Kanisa Lake.

Mungu kamwe hapendezwi na talaka lakini kwa kujua ugumu wa mioyo ya watu aliruhusu hili katika Agano la Kale, lakini anaweka wazi kuwa ikiwa mtu huyu ataoa tena basi anazini. Ikiwa mtu hawezi kubaki peke yake, basi angepasa kuuona ukweli juu ya umuhimu wa kutoshindwa kudumu katika ndoa, hivyo basi watafute neema ya Mungu ili ndoa hiyo iendelee kuwepo.

Tunatambua kuwa inawezekana kukawa na mambo mbalimbali ambayo yaweza kuleta mkanganyiko mkubwa, na hivyo basi, itabidi viongozi wa Kanisa kwa pamoja watoe maelekezo kwa kadiri tunavyopata hekima ya Mungu katika jambo husika.

**Marko 10:2-12**

KITENGO CHA FAMILIA

Familia nzuri ya Kikristo ni ile inayoendana na kanuni za Kibiblia na ambayo kila mmoja ndani yake anaelewa na kutimiza jukumu lake alilopewa na Mungu. Familia siyo taasisi iliyotengenezwa na mtu. Iliumbwa na Mungu kwa manufaa ya mwanaume, na mwanaume amepewa uwakili juu ya familia. Kitengo cha familia Kibiblia inajumuisha mwanaume mmoja, mwanamke mmoja – mwenzi wake – na watoto wao au watoto waliohalisiwa.

Familia ya ndugu na jamaa yaweza kujumuisha ndugu wa damu au ndoa kama vile wakwe, mpwa upande wa mume au mke, mabinamu, mashangazi, na wajomba. Moja ya kanuni za msingi za kitengo cha

familia ni kuwa inahusisha kujitoa kikamilifu kulikowekwa wakfu na Mungu kwa maisha yote ya wahusika. Mume na Mke wana jukumu la kushikamana, bila kuweka kando desturi njema zilizopo za utamaduni wetu. Ingawa talaka inafikiriwa na kutolewa sana kirahisi katika jamii yetu, Biblia inatuambia kuwa Mungu anachukia kuachana – **Malaki 2:16**.

Kwa kweli, hitaji la kwanza kwa wahusika wa familia ya Kikristo ni kuwa wote wawe Wakristo, wakiwa na mahusiano ya kweli pamoja na Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao. **Waefeso 5:22-26** inatoa maelekezo kwa waume na wake katika familia ya Kikristo. Mume anahitajika kumpenda mke wake kama vile Kristo anavyolipenda Kanisa, na mke anapaswa kumuheshimu mume wake na kujitoa kwa hiari kutii chini ya uongozi wa mume wake katika familia. Jukumu la uongozi la mume linapaswa kuanzia kwenye mahusiano yake binafsi na Mungu kiroho, kisha kuendelea kuelekeza mke wake na watoto katika kanuni za kimaandiko, kuiongoza familia katika kweli ya Kibiblia. Akina baba wanaelekezwa kuwalea watoto wao katika "adabu na maonyo ya Bwana" – **Waefeso 6:4**. Baba pia ana jukumu la kutoa kwa ajili ya familia yake. Asipofanya hivyo, "ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini" – **1 Timotheo 5:8**. Hivyo, mwanaume ambaye haweki juhudi kutunza familia yake hawezi kujiita kwa usahihi Mkristo. Hii haimaanishi kuwa mke hawezi kusaidia katika kutunza familia – **Mithali 31** inaonesha kuwa Mke mwema anaweza kwa hakika kufanya hivyo – lakini kimsingi jukumu la kutoa kwa ajili ya familia siyo lake; ni la mume wake.

Mwanamke alitolewa kwa mwanaume kwa dhumuni la kuwa msaidizi kwa mume wake – **Mwanzo 2:18-20** na kuzaa watoto. Mume na mke katika familia ya Kikristo wanapaswa kubaki waaminifu kila mmoja kwa mwenzake kwa kipindi cha maisha yote. Mungu anatamka usawa wa thamani katika mwanaume na mwanamke kuwa wameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu na hivyo wana thamani sawa mbele ya macho Yake. Hii haimaanishi, hata hivyo, kuwa wanaume na wanawake wana wajibu wa kufanana kabisa katika maisha. Wanawake ni wahusika zaidi

katika malezi na kutunza watoto, huku wanaume wameandaliwa vizuri zaidi ili kutoa mahitaji na kulinda familia. Hivyo, wana hadhi sawa, bali kila mmoja ana jukumu tofauti la kufanya katika ndoa ya Kikristo.

Ndoa ya Kikristo, iliyo msingi wa familia ya Kikristo, inafuata maelekezo ya Kibiblia kuhusu tendo la ndoa. Biblia inapingana na mtazamo wa kiutamaduni kuwa talaka, kuishi pamoja bila kuoana, na ndoa ya jinsia moja zinakubaliwa mbele ya macho ya Mungu. Tendo la ndoa lilivyoelezewa kulingana na viwango vya Kibiblia ni udhihirisho mzuri wa upendo na kujitoa. Nje ya ndoa, ni dhambi.

Watoto wanapewa wanapewa majukumu mawili katika familia ya Kikristo: kutii wazazi wao na kuwaheshimu – **Waefeso 6:1-3**. Kutii wazazi ni wajibu wa watoto hadi wanapofikia utu uzima, lakini kuheshimu wazazi wao ni wajibu wao katika maisha yote. Mungu ameahidi baraka zake kwa wale wanaoheshimu wazazi wao.

Inadhaniwa kuwa, wahusika wote katika familia ya Kikristo watakuwa wamejitoa kikamilifu kwa Kristo na utumishi Wake. Wakati mume, mke, na watoto wanatimiza jukumu walilopewa na Mungu, ndipo amani na mshikamano unatawala nyumbani. Bali, tunapojaribu kuwa na familia ya Kikristo pasipo kuwa na Kristo kama Kichwa au pasipo kukubaliana na kanuni za Kibiblia ambazo Mungu ametupatia kwa upendo, patakuwapo matatizo nyumbani.

KUBARIKI WATOTO

Ubarikio wa watoto ni kusanyiko lenye ishara linalofanywa na wazazi wa Kikristo mara baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Kwa ajili ya ubatizo wa maji mtu hupaswa “kumwamini” Yesu kwanza kabla ya kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa. Mtoto mdogo, hasa mtoto mchanga hawezi kuwa amefikia viwango vya kuweza kuamini na kwa msingi huu, hatuamini katika “ubatizo wa watoto wadogo”.

Ubarikio unakusudiwa kuwa tamko la hadharani linalotolewa na wazazi kuwa watamfundisha mtoto wao katika imani ya Kikristo na kufuta kuiweka imani hiyo ndani yao.

Kwa kawaida kusanyiko huitikia kwa kusoma au kwa namna nyingine kukubali kuwa, Kanisa kama familia, litaweka mkazo katika kutia moyo wazazi ili kuwalea watoto katika imani. Hakuna kinachomaanisha wokovu katika tendo hili, na inatofautiana kati ya kanisa moja na jingine.

Wazo la kuwaleta watoto kwa Bwana linapatikana katika Biblia – **Marko 10:13-16**. Hana alikuwa mke tasa ambaye aliahidi kuwa iwapo Mungu atampa mwana, angempa Mungu mtoto huyo – **1 Samweli 1:11**. **Luka 2:22** inaanza habari ya Mariamu na Yusufu wakimpeleka Yesu hekaluni baada ya siku arobaini ili 'wamweke kwa Bwana'. Hii ilizidisha jambo kidogo kwani ilihusisha sadaka, hata hivyo tena, katika tendo hili hakuna kinachomaanisha wokovu kwa kiwango chochote.

Ubarikio wa watoto siyo miongoni mwa kanuni mbili – ubatizo na meza ya Bwana – walizopaswa kufanya Wakristo katika Agano Jipya. Kama Wakristo, tunabatizwa na kushiriki katika meza ya Bwana kama udhihirisho wa nje na ishara ya hadharani ya kile Kristo alichokifanya ndani yetu. Huku ubarikio wa watoto siyo kanuni rasmi ya Kanisa, hakuonekani kutofautiana kokote na Maandiko ili mradi tu wazazi hawalitazami tendo hili kama hakikisho la wokovu wa mtoto.

*Sura ya 12*


# NINI KINATOKEA MWISHO

Somo juu ya "Siku za Mwisho" (Eskolojia) ni kubwa sana, tata na linalohitaji maelezo mengi, hivyo basi, kwa kusudio letu tutatoa maelezo kwa kifupi kwa kuweka tu msingi ambao waweza kujenga juu yake.

Uelewa wetu kuhusu matukio ya siku za mwisho yanategemeana na nafasi yetu katika "milenia" (Miaka 1000 ya kutawala Kristo). Kulingana na maandiko yanayohusiana na siku za mwisho yanavyotafsiriwa kutokea katika mtazamo huu.

Kuna nafasi 3 za msingi za milenia;

1. Kabla-milenia: Milenia itaanza katika ujio wa pili wa Kristo; huu ni wakati ujao.



Kabla-milenia inatetea yafuatayo;

- Utawala wa milenia unaanzia wakati wa ujio wa pili wa Yesu.
- Shetani ni mungu wa ulimwengu huu hadi atakaporudi Kristo, ni baada ya hapo TU ndipo atafungwa.
- Kristo atarudi Yerusalemu katika jinsi ya mwili na kutokea hapo anatawala.
- Kristo analeta mwisho wa tawala zote za kibinadamu na kuuweka ufalme Wake wa milele, uonekane wazi duniani.
- Watakatifu waliofufuka wanarudi na Kristo katika jinsi ya mwili ili kutawala pamoja naye.
- Shetani atafungwa na hatakuwa na ushawishi juu ya dunia hadi mwisho wa milenia.
- Shetani atafunguliwa mwishoni mwa milenia, atadanganya mataifa kuingia katika vita dhidi ya Kristo inayoitwa vita ya Gogu na Magogu ambapo mataifa yataangamizwa.
- Shetani atatupwa katika ziwa la moto.
- Wasio haki wote watakabiliwa na hukumu ya mwisho (Kiti cha Enzi cheupe) na kisha kutupwa katika ziwa liwakalo moto.
- Dunia hii kama tujuavyo inakuwa imeangamizwa na Kristo anatengeneza mbingu mpya na nchi mpya ambayo ni wenye haki PEKEE wamo ndani yake.


2. Ya-milenia: Hakuna umilenia, ni mfano wake tu.



Ya-milenia inatetea yafuatayo;

- Umilenia ni mfano tu.
- Kanisa lipo badala ya Israeli (hakuna juma la 70 la Danieli wala kusudi la kinabii lililobaki).
- Hakuna kipindi cha dhiki kuu (hii ilishakamilika katika mwaka wa 70AD wakati hekalu lilipoharibiwa).
- Hakuna utawala wa mpinga-Kristo (Nero alikuwa mpinga-Kristo katika kipindi kilichooneshwa hapa juu).
- Hakuna vita ijayo ya Armagedoni.
- Hakuna unyakuo wa Kanisa bali tu kuna ufufuo wa jumla wakati wa kurudi kwa Kristo.
- Shetani hafungwi kipindi cha milenia.
- Kanisa linatawala sasa pamoja na Kristo.

3. Baada-milenia: Milenia ni “zama ya dhahabu” ya maadili ya Kikristo inayoitimishwa na ujio wa mara ya pili wa Kristo. Tupo kwenye milenia hata sasa.



Baada-milenia inatetea yafuatayo;

- Kanisa litakuwa na utawala unaokua kwa kipindi hata utakapofikia kilele chake kwa kurudi kwa Kristo mara ya pili.
- Kanisa limekuwepo badala ya Israeli (hakuna juma la 70 la Danieli wala hakuna kusudi la kinabii lililobaki).
- Hakuna kipindi cha dhiki kuu (hii ilishakamilika katika mwaka wa 70AD wakati hekalu lilipoharibiwa).
- Hakuna utawala wa mpinga-Kristo (Nero alikuwa mpinga-Kristo katika kipindi kilichooneshwa hapa juu).
- Hakuna vita ijayo ya Armagedoni.
- Hakuna unyakuo wa Kanisa bali tu kuna ufufuo wa jumla wakati wa kurudi kwa Kristo.
- Shetani hafungwi kipindi cha milenia.
- Kanisa linatawala sasa pamoja na Kristo.
- Ulimwengu unaendelea kuwa bora na siyo mbaya zaidi (The world gets better not worse (kuteswa kwa Ukristo kumepungua).
- Kanisa litaufanya ulimwengu kuwa wa Kikristo, na kupelekea kuongezeka kwa dhamiri safi hadi atakaporudi Kristo.

**Tunaamini kuwa mtazamo wa kabla-milenia ni wa Kibiblia**

Tukiweka msingi katika mtazamo wa kabla-milenia, matukio yafuatayo bado yapaswa kutokea;

1. Kuinuka kwa wafalme 10 - **Ufunuo 13:1-10, 17:12-18** (watandawazi wanaotawala dunia).
2. Uasi mkuu na kuteswa kwa Ukristo - **2 Wathesalonike 2:1-12** (kama matokeo ya utawala wa utandawazi).
3. Unyakuo wa Kanisa - **1 Wathesalonike 4:13-18**
4. Vita ya **Ezekieli 38-39** (Israeli kuvamiwa na Urusi, Irani, Uturuki, Ethiopia, na Libya).
5. Chukizo la uharibifu - **Danieli 12:11** na **Mathayo 24:15** (shetani kuingia hekaluni na kujitangaza mwenyewe kuwa mungu).
6. Kutawala kwa mpinga-Kristo kwa miaka 3 1/2 - **Danieli 12:11**

7. Kuteswa kwa Israeli - **Mathayo 24:15-22**
8. Vita ya Armagedoni - **Ufunuo 16:13-16**
9. Kurudi kwa Kristo mara ya pili - **1 Wakorintho 15:23-26**

**KUMBUKA:** Ni muhimu sana kila mara kukumbuka yafuatayo kulingana na mafundisho ya "Siku za Mwisho";

1. Yesu PEKEE anaweka ufalme Wake kipindi cha kurudi kwake mara ya pili (hauwekwi na wanadamu).
2. Kwahiyo shetani ni mungu wa ulimwengu huu hadi atakapokuja Kristo mara ya pili.

**Makosa yanayotokea kwenye mitazamo ya Ya-milenia na Baada-milenia:**

***Theolojia ya Kutawala***

Theolojia ya Kutawala ni mjumuisho wa mifumo ya kitheolojia yenye inayoamini kwa pamoja kuwa jamii inapaswa kuongozwa hasa kwa sheria za Mungu kama zilivyowekwa wazi katika Biblia, na kuachana na sheria za kidunia. Mikondo miwili ya Theolojia ya Kutawala ni ". The two main streams of Dominion Theology are "Matengenezo ya Kikristo na Theolojia ya Ufalme Sasa". Ingawa inatofautiana sana katika mwelekeo wake wa jumla wa kitheolojia (wa kwanza ni wa Matengenezo zaidi na wa Kalvin-Mamboleo, wa pili ni wa Kiuamsho), inashirikiana mtazamo wa baada-milenia ambao Ufalme wa Mungu utawekwa duniani kwa njia ya kisiasa na (kwa namna mbalimbali) hata kwa njia za kijeshi.

Jina "Theolojia ya Kutawala" linatokana na **Mwanzo 1:28**, ambapo Mungu anampa mwanadamu "utawala" juu ya Dunia.

**KUMBUKA: ADAMU ALIPOANGUKA ALIPOTEZA UTAWALA WAKE NA UKACHUKULIWA NA SHETANI - Waefeso 2:1-2 & 2 Wakorintho 4:4.** Shetani ni mungu wa dunia

hii na ataendelea hivyo hadi Kristo atakaporudi mara ya pili, hadi itakapofikia hapo Kristo atachukua utawala na kuweka ufalme Wake – **1 Wakorintho 15:23-26**.

*Matengenezo ya Kikristo*

Mfano wa Utawalaji katika theolojia ya matengenezo ni Matengenezo ya Kikristo, inayotokana na mafundisho ya R.J. Rushdoony katika miaka ya 1960 hadi 1970. Theolojia ya Rushdoony imeweka shabaha yake kwenye theonomia (utawala wa Sheria ya Mungu), imani kuwa jamii nzima yapaswa kuongozwa kulingana na sheria zilizowaongoza Waisraeli katika Agano la Kale.

Matengenezo ya Kikristo ni theolojia ya matengenezo ambayo inaweka mkazo zaidi katika utawala wa Mungu juu ya uhuru na matendo ya binadamu, na inakanusha utendaji wa vipawa vya kihaiba katika siku za leo (kukoma); mitazamo hii yote inapingana na Theolojia ya Ufalme Sasa.

*Theolojia ya Ufalme Sasa:*

Theolojia ya Ufalme Sasa ni tawi la Theolojia ya Kutawala ambayo ina ufuasi katika mzunguko wa Kipentekoste na Kiuamsho na ikapewa umaarufu katika miaka ya mwishoni mwa 1980.

Theolojia ya Ufalme Sasa inasema kuwa ingawa shetani amekuwa mtawala wa dunia tangu anguko la mwanadamu, Mungu anatafuta watu ambao watamsaidia kurejesha utawala. Wale ambao wanajiweka wenyewe kwenye mamlaka ya mitume na manabii wa Mungu watachukua utawala wa falme za ulimwengu huu (milima 7).

Watangazaji wakuu wa hii harakati watetezi wa "Latter rain and New Apostolic Reformation".

**Makosa yanayotokana na Theolojia ya Ufalme Sasa:**

Imekuwa ni muhimu kuweka wazi makosa yafuatayo, kwa sababu ya ushawishi mkubwa katika Kanisa, na hasa katika Upentekoste na vikundi vya Uamsho.

*The Latter Rain Movement* (LRM)

LRM ilianza katika miaka baada ya Vita Kuu ya II ya Dunia na ikatiliwa mkazo zaidi na uamsho wa kiinjili uliotokea na Billy Graham akiwa mstari wa mbele, pamoja na Uamsho wa Uponyaji ulioongozwa na Oral Roberts, Jack Coe, na William Branham.

LRM ilileta shabaha mpya katika mambo ya kiroho ya Ukristo ikiwa ni pamoja na upewaji unabii, vita ya kiroho, na utafsiri wa Maandiko kitaipolojia ikiwa na msisitizo tofauti wa kieskatolojia.

Kipengele kikuu cha LRM iliyotarajiwa kingekuwa "udhihirisho wa Wana wa Mungu" au "Jeshi la Yoeli". LRM ilifundisha kuwa kwa kadiri mwisho dahari unavyokaribia, "washindi" watatokea ndani ya Kanisa.

Hawa Wana wa Mungu waliodhihirishwa, ndio ambao wamefikia kimo cha Yesu Kristo na wamepokea Roho pasipo kipimo. Wangekuwa kama Yesu alivyokuwa akiwa duniani na wangepokea kiasi cha vipawa kiungu, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kubadili maeneo wanapopatikana kimwili, kuzungumza kwa lugha yoyote kwa njia ya Roho Mtakatifu, na wangeweza kufanya uponyaji na miujiza mingine. Wangeweza kumaliza kazi ya Mungu, kurejesha nafasi kuu ya mwanadamu kama ambavyo hapo awali alipewa na Mungu katika **Mwanzo 1:28** na kwa kufikia kimo cha Kristo wangeingia katika utawala Wake wa milenia. Msemo uliokithiri kuhusu Yesu kama "muundo" Mwana na unaotumiwa "ndinyi miungu" - **Zaburi 82:6** kwa hili kundi la waamini.

Watangazaji wenye kasi sana walikuwa ni Manabii wa Kansas City (Paul Cain, Bob Jones na Mike Bickle) na New Apostolic Reformation (NAR) ambayo kwa sasa ni watetezi wakubwa. C. Peter Wagner akiwa ameweka mizizi katika Latter Rain Movement alijipa nafasi kama "Mtume Mkuu" wa NAR, akiwa na ajenda kali ya utawala.

Tuseme kwamba Wana wa Mungu waliodhihirishwa wanatarajiwa kutawala dunia wakati wa milenia hadi hapo mwishoni ambapo kila mwanadamu atarejeshwa katika maelewano na Mungu.

New Apostolic Reformation (NAR)

NAR ni harakati katika Ukristo wa Protestanti ambao kwa kiasi kikubwa inahusiana na harakati za Upentekoste na Uamsho. Tasnifu ya

msingi inasisitiza kuwa Mungu anarejesha huduma ya Manabii na Mitume (Sawa na Mitume 12 na Paulo, aliyepokea ufunuo ufunuo mpya uliokubalika pia kama maandiko). Hii ni kufuru inapaswa kukataliwa - **Wagalatia 1:6-9** na kulingana na andiko hili, hawa watu yapasa walaaniwe.
Kulingana na Wagner, "Zama za pili za utume zilianza mwaka 2001", ambapo kulingana na yeye, huduma zilizopotea za "Manabii" na "Mitume" zilirejeshwa, katika zama hii.

Spiritual Warfare Movement (SWM)
SWM inajumuisha utendaji mbalimbali wa matendo ambayo hayapo kibiblia ambapo shetani na mapepo hupigwa vita, kwa kutumia mbinu mbalimbali kulingana na kikundi kinavyoamini, lakini kwa maombi kabisa.
Kulingana na C. Peter Wagner, "uwekaji katika ramani kiroho" inahusisha utafiti na maombi ili kuweka watu mahususi ambao wanatuhumiwa kwa ushirikina, au watu, vikundi, au maeneo ambayo yanadhaniwa kuwa yaliyoathirika kwa ushirikina au yamejawa na mapepo, ambapo vita ya kiroho inapasa kuwepo. Peter Wagner anadai kuwa aina hii ya vita ya kiroho ilikuwa "haijulikani vizuri kwa Wakristo wengi kabla ya miaka ya 1990". Kulingana na Wagner, mbinu ya msingi ni kutumia "uwekaji katika ramani kiroho" kuonesha maeneo, watu waliojawa na mapepo, wataalamu wa uchawi kama vile waganga wa kienyeji na ma-freemason, au sanamu za kichawi, sanamu za watakatifu wa kikatoliki, ambazo baada ya hapo hutajwa na kupigwa, kwa kutumia mbinu mbalimbali kuanzia kwenye maombi makali hata kufikia kuchoma kwa moto.
Vita ya kiroho imekuwa kipengele maarufu katika baadhi ya makanisa ya kipentekoste na uamsho. Dhana hii imeingia hasa katika historia ya Upentekoste, hasa kupitia Kitabu cha Jessie Penn-Lewis 'Vita juu ya Watakatifu iliyoinuka kutokana na Uamsho wa Welsh katika kipindi cha mwanzoni mwa karne ya Ishirini'. Hatahivyo, Jessie Penn-Lewis anahubiri vita ya kiroho tofauti kabisa na iliyohubiriwa na wimbi la tatu la harakati za Uamsho wa leo - haswa C. Peter Wagner na Cindy Jacobs. Makosa mengine ambayo yanahusishwa ni pamoja na; uponyaji

wa ndani, kuvunja laana za kurithi, kutambua na kuweka vita juu ya maeneo ya anga za kiroho, kutia mafuta vigingi vitakavyowekwa katika maeneo ya kimkakati na kuzika Biblia katika viwanja. Wengine wamejipumzisha kwenye vitendo visivyo na akili na vya bure vya "kumfunga shetani na mapepo, kufanya maandamano ya Yesu na makusanyiko ambapo vita inafanyika dhidi ya ulimwengu wa kipepo kwa kuzungumza katika anga, kukemea, kutangaza (hata kunguruma kama samba) na kufunga. Ni jambo la kusikitisha kuwa nyuma ya haya mafundisho yote na vitendo potofu, injili ya mafanikio imepewa msukumo. Yesu na mitume walituonya kuhusu kutokea kwa manabii wa uongo katika siku za mwisho.

Makosa yaliyoorodheshwa hapa juu ni wazi kuwa siyo ya Kibiblia na yamepelekea kwenye mkanganyiko, kuumiza, kukosa kuwa na uaminifu na hata kukataliwa kwa Injili ya kweli.

Maelezo ya mwanzo ya kimandiko kwa ajili ya dhana ya vita ya kiroho yanaweza kupatikana katika **Waefeso 6:11-18**, ambapo Paulo kwa kutumia tamathali za semi anahimiza Wakristo kujivika silaha za kivita zinazofanana na zile za askari wa Kirumi. Hatahivyo, ni vema sana kukumbuka kuwa wazo hili la "silaha" kutoka kwa Mungu, ikiwa ni pamoja na "chapeo ya Wokovu" na "dirii ya Haki kifuani" ambazo Paulo anazitaja, zimejumuishwa pia katika **Isaya 59:17**, iliyotangulia kuwepo karne nyingi kabla ya Jamhuri ya Rumi na jeshi lake kubwa. **Zaburi 18** inatoa picha ya karibu ya vita ya kiroho (nguvu ya kiungu ya Mungu inashinda mikakati ya adui Zake), na inatoa marejeo mbalimbali kuhusu kutiwa nguvu kwa ajili ya pambano – mstari wa **32, 33, 36, na 39**. **Zaburi 17:5, 140:4** na **149:6-9** pia zinadokeza kuhusu vita hii.
Uwanja wa vita hii ulihamishwa kutoka katika ulimwengu wa mwili na kufanywa kuwa katika ulimwengu wa roho - **Waefeso 2:5-6, 1 Wakorintho 15:24, Waefeso 1:21, 3:10, 6:12, Wakolosai 1:16, 2:10** na **2:15**).

**1 Wakorintho 10:3-6** inafundisha kwa uwazi kabisa kuwa vita ya kiroho ni ile inayochukua nafasi katika mawazo ya akili na ni wajibu wa kila mtu.
Ushindi wetu umeshapatikana katika Kristo, hatuhitaji kupambana na shetani na mapepo yake katika jinsi ya mwili, kwani tumekuwa viumbe vipya na zaidi ya washindi katika - **2 Wakorintho 5:17** na **Warumi 8:37**.

**Sasa ni lini Kanisa litanyakuliwa?**
Manabii wengi wa Agano la Kale na hata Paulo, Petro, na Yohana wanazunumzia juu ya "Siku ya Bwana" kama siku ya giza, kisasi, huzuni, ghadhabu. Hii siyo siku fulani maalum bali ni kipindi cha muda kuanzia kufunguliwa kwa Muhuri wa 6 - **Ufunuo 6:12-17** na kuhitimishwa wakati wa hukumu kutoka "Kiti cha Enzi Cheupe". "Siku ya Bwana" ni kipindi ambacho Yesu anaanza kumwaga ghadhabu Yake **(Ufunuo 6:16-17)** juu ya ulimwengu, anarudi kuangamiza maadui zake katika Armagedoni na kuweka mwisho wa tawala za wanadamu na kisha kuweka ufalme Wake wa milele. Ufalme unaanzishwa duniani ambapo ulimwengi unaongozwa na Yesu kwa fimbo ya chuma na kuhitimishwa kwa hukumu kutoka "Kiti cha Enzi Cheupe". Ndipo Siku ya Bwana inafikia mwisho na Yesu anatengeneza mbingu mpya na nchi mpya.
Tunaamini Kanisa litasalimika "Siku ya Bwana"kama Paulo anavyofundisha kuwa "Mungu hakutuweka kwa hasira yake" - **1 Wathesalonike 5:1-11.** Tunaona katika taipolojia ya Biblia kuwa Mungu mara zote amekuwa na mpango wa uokoaji kabla ya kumwaga ghadhabu yake; kwa mfano, Nuhu na Lutu. Hivyo, kilicho wazi katika maandiko ni kuwa Kanisa litanyakuliwa kabla ya "Siku ya Bwana".

Siku hii inakuja upesi; sisi kama Kanisa twapaswa kurudi katika mafundisho ya mitume katika mguso wenye bidii kwa ajili ya imani ambayo mara moja na kwa ajili ya wote ilipewa watakatifu kama alivyofundisha Yuda. Ni wakati wa kutambua na kukesha. Kutembea kwa kujisalimisha kikamilifu na kumtii Kristo kwa kadiri tuisubiriavyo

kwa maombi “Siku ya Bwana” iliyo kuu na ya kutisha itakayokuja juu ya ulimwengu. Na kwa mwisho huu, Paulo anakumbusha Kanisa kuwa sisi tu wana wa “Nuru” na kuwa tutasalimika katika “Ghadhabu” itakayokuja - **1 Wathesalonike 5:1-11**

Maombi yetu ni kuwa Roho Mtakatifu akupe ufunuo na ufahamu wa maandiko na kuweza kupata neema ya Mungu isiyoshindwa unavyoendelea kutembea katika nuru ya mafundisho ya mitume.
Kwa viongozi wa Kanisa, Mungu na awape hekima kuu katika ujenzi wa Kanisa juu ya msingi huu.

# Kesha! Simama imara katika imani! Fanya kiume! Kuwa hodari!

**1 Wakorintho 16:13**